epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Novemba 7, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii

ISSN 0856 • Na. 0581853
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

## WATAFITI MUHIMBILI...

# Viuatilifu shambani vimeanza kudhuru



• **Chanzo** ongezeko la saratani, kisukari, matatizo ya uzazi... *Uk.2*



"Zimbabwe iko tayari kufanya kazi na wewe na watu wa Marekani ili kujenga ulimwengu bora wenye mafanikio na amani zaidi duniani.

**Emmerson Mnangagwa (ZIMBABWE)**



"Tunatazamia kwa hamu kushirikiana kwa karibu na Marekani kwenye urais wetu wa G20 mwaka wa 2025, ambapo Marekani itaturithi mwaka wa 2026.

**Cyril Ramaphosa (AFRIKA KUSINI)**



"Ninatarajia kufanya kazi nanyi katika miaka ijayo, kama washirika wa karibu zaidi, tuko bega kwa bega kutetea maadili yetu ya pamoja ya uhuru, demokrasia na biashara.

**Keir Starmer (Waziri Mkuu Uingereza)**



"Tuko tayari kufanya kazi pamoja kama tulivyofanya kwa miaka minne, kwa amani na ustawi zaidi.

**Emmanuel Macron (UFARANSA)**



"Natarajia kuimarisha uhusiano wetu na ushirikiano wa kimkakati na kuimarisha juhudi zetu za pamoja za kukuza usalama na utulivu katika kanda na ulimwengu.

**Sheikh Tamim bin Hamad Al Thani (EMIR WA QATAR)**



"Ushindi wako (Trump) ni wa kihistoria. Ninakutakia heri na fanaka katika uongozi wako.

**Evariste Ndayishimiye (BURUNDI)**



# Marais duniani walivyopokea ushindi wa Trump

UKURASA 19

UKURASA WA 2

**Wakulima** korosho wafunga barabara kuu Lindi - Mtwara kushinikiza walipwe

UKURASA WA 3

**Ajira** kwa watu 600,000 nchini zazalishwa nusu ya mwaka huu

UKURASA WA 3

**Sheria** kudhibiti bodaboda yaiva, kutua bungeni wakati wowote

UKURASA WA 22

## DIAZ AMKOSHA SLOT LIVER



KESI KUCHOMA MKE KWA MKAA

## Sajenti: Mshtakiwa aliamua kusema ukweli ili awe huru

UKURASA 4




Skani hapa kutembelea chaneli yetu

# Watafiti MUHAS wabaini shida matumizi ya viuatilifu kuzalisha mboga za majani

**Na Grace Mwakalinga**

UTAFITI uliofanywa na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) umebaini ongezeko kubwa la matumizi ya viuatilifu katika kuzalisha mboga za majani, hata kuchangia ongezeko la magonjwa hatari nchini.

MUHAS wamebaini ongezeko hilo limepiku matumizi ya viuatilifu katika kilimo cha pamba na kahawa ambacho kwa muda mrefu kilitumia zaidi kemikali hizo.

Matokeo ya utafiti huo uliofanywa katika mikoa yote nchini, yanaonesha matumizi ya viuatilifu kwenye uzalishaji mboga za majani yanachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la magonjwa yasiyoambukizwa kwa binadamu kama vile saratani, kisukari na matatizo ya uzazi.

Mhadhiri na Mtafiti Mwandamizi wa MUHAS, Dk. Vera Ngowi, wakati wa kongamano la kujadili viuatilifu vya kuulia wadudu na afya nchini na Afrika Mashariki lililofanyika MUHAS, alisema matumizi ya viuatilifu kwenye kilimo cha mboga za majani yanahatarisha afya za wananchi.

Alishauri kuongeza kampeni ya kutoa elimu na uhamasishaji kuhusu hatari za matumizi ya viuatilifu kwa afya ya binadamu.

Alisema mamlaka pia zinapaswa kuweka kipaumbele kwa utekelezaji thabiti wa kanuni za viuatilifu ili kuondoa vilivyopigwa marufuku na kuongeza ufuatiliaji wa kanuni.

"Miaka ya nyuma kulikuwa na matumizi makubwa ya viuatilifu kwenye mazao ya pamba na kahawa. Hali imebadiika, uzalishaji wa mboga za majani hivi sasa unatumia kiwango kikubwa, jitihada zinahitajika kukabiliana na suala hilo ili kunusuru afya za wananchi," alisema Dk. Ngowi.

Aliwashauri wakulima kutumia mbinu mbadala zisizo na kemikali za kudhibiti visumbufu kama vile usimamizi ili kupunguza utegemezi wa kemikali zenye kemikali hatari za viwandani pamoja na kuongeza ushirikiano baina ya wakulima, watumiaji na mashirika ya kijamii ili kuongeza uelewa na kukuza kampeni za msingi za mabadiliko ya sheria za usimamizi wa viuatilifu.

"Pia tuna jukumu la kutoa motisha kwa wakulima kufanya kilimo hai na mbinu nyingine zinazopunguza athari kama vile viuatilifu vya kibaiolojia," alisema.

Makamu Mkuu wa MUHAS, Prof. Appolinary Kamuhabwa (pichani), alisema waliamua kufanya utafiti wa athari za viuatilifu kwa afya ya wananchi kwa kuwa hilo ni eneo ambalo halijafanyiwa utafiti kulinganisha na mengine.



Alisema utafiti huo ambao wameufanya kwa ushirikiano na wataalamu wa Norway, kikiwamo Chuo Kikuu cha Oslo na Ubalozi wa Ufaransa nchini, unalenga kuangalia athari za kiafya kwa binadamu kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya viuatilifu na mabadiliko ya tabianchi.

"Tunaangalia maeneo ambayo yanaathiri afya ya binadamu, yakiwamo matumizi yasiyo sahihi ya viuatilifu. Baada ya kongamano hili, tutengeneze mapendekezo kama vile sera au aina gani ya elimu itolewe kwa makundi mbalimbali ya watu.

"Utafiti huu pia unalenga kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanasababisha vitu mbalimbali kubadilika, hata matumizi ya viuatilifu, aina za wadudu, magonjwa ya binadamu na mazao, hivyo tunaangalia ni kwa namna gani viuatilifu vitatumiwa kwa usahihi," alisema Prof. Kamuhabwa.

Joseph Bilago, Mkuu wa Afya Kazini, aliyemwakilisha Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, alisema kongamano hilo linalohusu matumizi ya viuatilifu kwenye shughuli za kilimo, afya na mifugo, litasaidia kuona namna matumizi hayo yanakuwa bora katika kulinda afya ya jamii na kupata mazao yanayozingatia matumizi sahihi ya viuatilifu hivyo.

"Viuatilifu vinatumika kwenye kilimo na kukabiliana na magonjwa kama vile malaria, vinatumika kuua viluilui vya mbu, hivyo kuna faida za matumizi hayo lakini kuna hasara pia endapo havitatumika ipasavyo hasa katika uzalishaji mboga na matunda kama nyanya, vitunguu, mboga za majani na kukuza mifugo," alisema Bilago.

Aliongeza kuwa matumizi ya viuatilifu hayakwepeki, hivyo ni vyema wananchi wakazingatia matumizi bora ya viuatilifu ili kulinda afya za wananchi, mimea, wanyama na mabadiliko ya tabianchi.






## Wakulima korosho wafunga barabara kushinikiza walipwe

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WAKULIMA wa korosho, kata ya Ndanda wilayani Masasi, mkoani Mtwara wamefunga barabara kuu kutoka mjini Masasi kuelekea Lindi na Mtwara wakishinikiza kulipwa fedha za korosho ambazo waliuza kwenye mnada wa kwanza, pili na watatu na hawajalipwa.

Wakulima hao walifunga barabara hiyo kwa kuweka magogo na mawe na kusababisha magari yanayofanya safari kutoka Masasi, Lindi na Mtwara kukwama kwa saa tatu.

Wakizungumza na waandishi wa habari katika eneo hilo, wakulima hao walisema wanahitaji kulipwa fedha zao za korosho walizouza katika minada iliyofanyika tangu kuanza kwa msimu wa zao hilo.

Walisema wanashangazwa kuona Chama Kikuu cha Ushirika Masasi-Mtwara na Nanyumbu (MAMCU), kuchelewesha malipo ya korosho za wakulima licha muda husika wa wakulima kulipwa kupita.

Juma Athumani, mkulima wa kata ya Ndanda, alisema wanaomba serikali kuingilia kati jambo hilo na kuhakikisha malipo yao ya korosho wanalipwa.

"Tumeamua kufunga barabara ili kushinikiza serikali na vyombo vinavyopaswa kulipa fedha zetu tunalipwa, vinginevyo hapa hatutoki mpaka kieleweke," alisema Athumani.

Ayubu Michael, mkulima kata ya Ndanda alisema wapo wakulima hawajalipwa fedha zao tangu kufanyika kwa mnada wa kwanza hadi kufikia mnada wa tatu na hawajui sababu inayokwamisha kutolipwa hadi sasa.

Asha Salumu alisema, wakulima wanachotaka ni kulipwa fedha zao na kuhoji tangu wameuza mazao yao hadi sasa hawajalipwa fedha zao huku muda wa kulipwa ukiwa umepita.

Alisema kuwa wakulima wa vyama vikuu vya jirani na Masasi wanalipwa fedha zao kwa wakati, lakini wa Masasi hawajalipwa hadi sasa.

Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Lauter Kanoni, alipozungumza na wakulima hao, aliwataka kuwa na subira wakati serikali ikiendelea kulifanyia kazi suala hilo.

"Serikali imelichukua na kuanza kulifanyia kazi suala hilo na wapo wakulima ambao wameshaanza kulipwa fedha zao tayari hivyo muwe watulivu," alisema Kanoni.

Kanoni alisema tayari serikali imeshakutana na viongozi wa vyama vya ushirika, mameneja wa benki na mitandao ya simu ambao wote kwa wanahusika kuwalipa wakulima ili kujadili changamoto ya hiyo ya kuchelewa kwa malipo ya korosho.

HABARI KITAIFA

# Ajira 600,000 zazalishwa miezi saba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATI ya Januari hadi Julai mwaka huu, ajira 607,475 zimezalishwa nchini ikiwa ni sehemu ya jitihada za serikali kufikia lengo la kuzalisha ajira milioni nane lililomo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya 2020-2025.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi aliyasema hayo bungeni jana alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Esther Maleko aliyetaka kujua serikali inatumia mbinu gani kuhakikisha watanzania wengi wanapata ajira nje ya nchi na juhudi zinazofanywa kufikia lengo la ilani la upatikanaji ajira milioni nane.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema lengo la serikali ni kutoa ajira milioni 1.2 kila mwaka.

"Njia ya pili inahusisha kutumia balozi zetu kutafuta nafasi za kazi kwa watanzania kwenye maeneo hayo. Tatu, wanadiaspora wa Tanzania pia ni sehemu ya mkakati wetu wa kupata fursa za ajira kwa watanzania," alisema.

Katambi alisema watanzania pia wanapata ajira nje ya nchi kwa juhudi binafsi kulingana na sifa zao za kielimu au vigezo vingine kama vile kuwa wanamichezo au kuwa na vipaji mbalimbali.

"Njia nyingine ni kupitia taasisi za elimu, wizara na vyuo vikuu ambako baadhi ya watanzania wanapata ajira nje ya nchi, zikiwamo nafasi za utafiti na fursa kupitia mashirika ya Umoja wa Mataifa. Kwa mfano, Dk. Faustine Ndugulile," Naibu Waziri alisema.

Katambi pia alisema serikali itafanya Utafiti Jumuishi wa Nguvu Kazi (ILFS) na Utafiti wa Mapato ya Ajira kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Benki ya Dunia.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalumu (CHADEMA), Grace Tendega, alihoji kuhusu mkakati wa serikali kubaini fursa za ajira nje ya nchi na kuzifikisha kwa watanzania.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema serikali tayari imeanza kutekeleza mpango maalumu kupitia Kitengo cha Huduma za Ajira Tanzania (TaESA) ili kubaini ajira zinazotangazwa mtandaoni na kuwafikia watanzania katika kanzidata, hata kuwasaidia kwa mafunzo ili kuhakikisha wanastahili kupata ajira hizo.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Shally Raymond alihoji wahitimu wangapi wa vyuo wanafanya kazi ya kujitolea na wangapi wameajiriwa na kujiajiri baada ya kujitolea.

Naibu Waziri Katambi alisema serikali ilianza rasmi kuratibu utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Mafunzo ya Uzoefu wa Kazi kwa Wahitimu mwaka 2019/20 na tangu kuanza utekelezaji programu hiyo, wahitimu 21,280 wamenufaika. Kati yao, wanaume ni 11,281 na wanawake ni 9,999.

Alisema miongoni mwa wanufaika hao, 3,772 wamepata kazi, wanaume wakiwa ni 2,265 na wanawake 1,507.

## Sheria yaja kuwabana bodaboda

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema ipo katika hatua za mwisho kuwasilisha bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973, ambao pamoja na mambo mengine, utaweka sharti la kuvaa kofia ngumu abiria na dereva wa bodaboda.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Asha Abdallah Juma.

Asha alihoji lini serikali itakuja na kipengele kwenye Sheria ya Usalama Barabarani cha kulazimisha uvaaji wa kofia ngumu kwa abiria na madereva wa bodaboda.

Sillo akijibu swali hilo, alisema sheria iliyopo sasa ina upungufu na hailazimishi abiria kuvaa kofia ngumu na kumhakikishia mbunge huyo kuwa katika maboresho ya sasa ya sheria hiyo jambo hilo limezingatiwa na sasa itakuwa ni lazima kuvaa kofia ngumu kwa abiria na dereva wa bodaboda.

Katika swali la msingi, Mbunge Viti maalum (CCM), Amina Ali Mzee, alihoji lini serikali itaanza kuweka sheria na uratibu mzuri wa kupunguza ajali za barabarani zinazotokana na uzembe wa madereva.

Akijibu swali hilo, Sillo alisema Jeshi la Polisi kupitia kikosi cha Usalama Barabarani kwa sasa inasimamia masuala ya usalama barabarani kwa kutumia Sheria ya Usalama barabarani Sura 168 ya mwaka 1973 kama ilivyo fanyiwa marejeo mwaka 2002.

"Katika mkakati wa kuboresha sheria hii ili kupunguza ajali za barabarani serikali imekusanya maoni kutoka kwa wadau na sasa inamalizia kuyafanyia kazi na baada ya hapo itawasilisha muswada wa sheria bungeni," alisema.



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, CPA Amos Makalla akizungumza na Wanachama pamoja na Viongozi wa chama hicho, Wilaya ya Ilala katika Ukumbi wa Mwigo Tabata jana. **PICHA: CCM**

## Mbunge ahoji raia wa kigeni kuwa meneja rasilimaliwatu wa Dangote

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Mtwara Mjini (CCM), Hassan Mtenga amehoji serikali sababu ya raia wa Nigeria kuajiriwa kama Meneja Rasilimaliwatu wa Kiwanda cha Saruji Dangote mkoani Mtwara ilhali sheria inakataza.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alisema suala hilo ni la muda mrefu -- lina miaka mitatu na meneja huyo yupo na kuhoji ni sababu gani zinakwamisha kuondolewa kwake.

"Ninaomba twende kwenye kiwanda cha Dangote akaone uhalisia wa jambo hili tunalozungumza," alisema.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alisema malalamiko yanayotolewa na mbunge yalishafika wizarani na kufanyiwa kazi.

"Kwa kuzingatia Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni, Sura 436 na Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Na. 10 ya mwaka 2022, ofisi ilifanya ukaguzi maalum katika kiwanda hicho tarehe 23 na 24, Septemba, 2024 ili kujiridhisha na ukweli wa malalamiko haya na utekelezaji wa Sheria za Kazi kwa ujumla. Serikali ilithibitisha malalamiko hayo," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za serikali, wanaendelea kushughulikia suala hilo na litakapokamilika, hatua stahiki zitachukuliwa.

Alisema serikali haina kigugumizi kuchukua hatua na kwamba wamechelewa kutokana na kubaini kuna uvunjifu wa sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai.

"Tayari polisi inaendelea kufanya uchunguzi wa makosa yaliyotendeka, sambamba na Idara ya Uhamiaji na Ofisi ya Waziri Mkuu tunaendelea kuyashughulikia, kama tungechukua hatua haraka kuna makosa ya jinai ambayo tungewanyima haki walitendewa," alisema.

KESI KUCHOMA MKE KWA MKAA

# Sajenti: Mshtakiwa aliamua kusema ukweli ili awe huru

Na Grace Gurisha

SAJENTI William Christopher (51) amedai mahakamani kuwa mshtakiwa Khamis Luwongo (38) anayedaiwa kumuua mkewe Naomi Marijani na kisha kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa, aliamua kusema ukweli kwa madai kuwa anataka kuwa huru.

Pia amedai alikatisha kumchukua maelezo ya onyo yaliyoanza kuanzia saa tano asubuhi hadi saa saba mchana, baada ya kueleza jinsi alivyomuua mke wake na kumchoma moto nyumbani, hivyo ikawabidi wahamie eneo la tukio.

Sajenti Christopher alidai hayo jana mbele ya Jaji Hamidu Mwanga wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati akitoa ushahidi dhidi ya mshtakiwa huku akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Yasinta Peter.

Alidai kuwa Julai 16, 2019, akiwa ofisini kwake Kanda Maalumu Dar es Salaam - Kitengo cha Uhalifu wa Mtandao, aliitwa na bosi wake ASP Ahmed Makelle ili awakutanishe na mshtakiwa kumhoji kuhusiana na mawasiliano baina yake na mkewe.

"Nilipewa utambulisho na ASP Makelle kuwa 'huyu ndiye mume wa Naomi aliyepotea, kuanzia hapo nikamjua, nikampeleka ofisini kwangu, nilikuwa mimi na yeye tu.

"Nikaanza kumwuliza maswali, akaniambia anatumia namba ya simu 0714 812530 na ya mke wake ni 0655 527203 na mke wake alipotea tangu Mei 15, 2019, asubuhi hadi siku hiyo (Julai 16, 2019," alidai Sajenti Christopher.

Alidai kuwa alimwuliza mshtakiwa kama mkewe Naomi aliondoka na simu zake na laini? Na pia alimwuliza kama walishawahi kuwasiliana kwa kipindi chote hicho, akasema walikuwa wakitumiana ujumbe mfupi.

"Nikamwuliza 'mbona zipo kwenye handset' moja unazozitumia wewe? Akashindwa kunipa jibu na alishindwa kunijibu kama walishakutana tena, ndiyo akatoweka kwa mara ya pili," alidai Sajenti Christopher.

Baada ya kushindwa kujibu maswali hayo, alimweleza Sajenti Christopher, akimnukuu kwamba alisema "ngoja tu nikueleze ukweli kwa sababu hata nikinyamaza siwezi kuwa huru". Akadai alimuua mkewe Naomi.

Kwa kauli hiyo ya mshtakiwa Luwongo, maarufu Meshack, ilitoa mabadiliko ambayo ilimbidi Sajenti Christopher atoke hapo, mshtakiwa akahojiwe kwa kuandikwa maelezo ya onyo kwa kuwa amekiri kufanya uhalifu wa kumuua mke wake.

"Nilianza kumhoji kuanzia saa tano asubuhi ya Julai 16, 2019, ambapo tulisitisha mahojiano saa saba mchana baada ya kueleza tukio alilifanya nyumbani kwake Gezaulole.

"Nilirudi kwa bosi wangu ASP Makelle kumweleza kuwa mshtakiwa amekiri kosa, wanajiandaa kwenda nyumbani kwake, walipofika alionesha eneo lote la tukio hadi sehemu alipomchomea na alipofukia mabaki na majivu ya mwili wa marehemu," alidai.

Alidai kuwa baada ya kumaliza tukio hilo, walirudi kituo cha polisi saa 5:45 usiku, aliandika maelezo ya nyongeza, walimaliza saa 6:20 usiku.

Jaji Mwanga alipokea maelezo hayo ya onyo ya mshtakiwa kama kielelezo namba moja katika kesi hiyo.

Katika kesi hiyo ya mauaji namba nne ya mwaka 2019, mshtakiwa Luwonga ambaye ni Mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam anadaiwa Mei 15, 2019, akiwa Gezaulole, Kigamboni, Dar es Salaam, alimuua Naomi Marijani.



Wakazi wa kijiji cha Masuguru, kata ya Kwamkabara, wilayani Muheza, mkoani Tanga, wakiwa wamepanga foleni ya kuchota maji, jana, kutokana na bidhaa hiyo kuwa adimu kijijini hapo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Miradi 63 yasajiliwa biashara ya kaboni

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis amesema serikali imesajili miradi 63 ya biashara ya kaboni kupitia sekta mbalimbali.

Khamis aliliarifu Bunge jijini Dodoma jana juu ya usajili huo wakati akijibu swali la Mbunge wa Amani, Abdul Yussuf Maalim aliyetaka kujua mpango wa serikali kupanua wigo wa biashara ya kaboni ili kupunguza uharibifu wa ukataji misitu nchini.

Naibu Waziri Khamis alitaja sekta zilizo katika miradi iliyosajiliwa ni pamoja na kilimo (asilimia nane), nishati (asilimia 33), misitu (asilimia 51), mifugo (asilimia tano) na usimamizi wa taka (asilimia tatu).

Alisema kuwa kati ya miradi iliyosajiliwa kupitia sekta ya misitu, minne inahusisha shughuli za upandaji miti, miradi 20 ni kwa ajili ya kupunguza uharibifu na upotevu wa misitu na miradi mitano ni kwa ajili ya kurejesha uoto wa asili.

Khamis pia alieleza kuwa serikali inaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia (2024 – 2034) ambao unahamasisha matumizi ya nishati safi za kupikia, ikiwamo gesi asilia, nishati jadidifu, mkaa mbadala na umeme ambazo zinaweza kuchangia katika biashara ya kaboni na kupunguza matumizi ya kuni na ukataji misitu.

Alisema serikali pia imeandaa na inatekeleza Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu 2024 na Mkakati wa Utekelezaji Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu (2024 – 2034).

# Kodi kupunguzwa uagizaji magari yenye mfumo wa gesi

Na Augusta Njoji, DODOMA

SERIKALI inaendelea kuangalia namna ya kupunguza au kuondoa kodi nyingine za uagizaji magari yenye mfumo wa gesi ili kuhamasisha matumizi ya gesi asilia.

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu (CHADEMA), Grace Tendega.

Mbunge huyo alitaka kujua mpango wa serikali kupunguza baadhi ya kodi ili watanzania wengi waingize magari yenye mfumo wa nishati ya gesi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kapinga alisema serikali kupitia bajeti yake ya mwaka 2023/24, ilitoa msamaha wa Kodi ya Ushuru wa Forodha asilimia 25 kwa injini za magari yanayotumia gesi asilia yanapoingizwa nchini.

Alisema serikali pia inaendelea na hatua mbalimbali za kuhamasisha sekta binafsi kutoka ndani na nje ya nchi kuwekeza kwenye viwanda vinavyotengeneza vipuri vinavyotumika katika kufunga mfumo wa matumizi ya gesi asilia kwenye magari na mitambo nchini.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema majibu hayo yanaonesha hakuna kiwanda kinachotengeneza vipuri nchini kutoka mfumo wa mafuta kwenda wa gesi na kuhoji wamepatikana wawekezaji wangapi baada ya sekta binafsi kushirikishwa kutengeneze vipuri hivyo.

"Serikali haioni haja ya kupunguza au kuondoa kodi kabisa katika vipuri vinavyoingizwa nchini," mbunge huyo alihoji.

Akijibu maswali hayo, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba alisema serikali imechukua hatua ambapo kwa mwaka 2024/25, imezingatia kupunguza kodi kwenye magari na vipuri vinavyotumia gesi.

"Hata hivyo, tumepokea maoni ya mbunge na tutaendelea kuyafanyia kazi hata katika mwaka wa fedha 2025/26 ambao tumeanza maandalizi ya kuandaa hatua za kikodi mpya na msukumo wa serikali ikizingatiwa Rais Samia Suluhu Hassan ni kinara ya matumizi ya nishati safi," alisema.

Mbunge wa Viti Maalumu (CHADEMA), Esther Matiko, akiuliza swali la nyongeza, alisema katika kuhamasisha matumizi ya gesi kwenye magari na mzigo mkubwa upo kwenye malori na mabasi na kwamba kuna vituo 14 ambavyo vinabadili magari ya petroli pekee kwenda mfumo wa gesi.

Alihoji mkakati wa serikali kupunguza gharama za usafiri na usafirishaji kwa kuweka kituo cha kubadili magari ya dizeli.

Naibu Waziri Kapinga, akijibu swali hilo, alikiri kuwa hivi sasa vituo vingi ni vya kubadilisha mfumo wa petroli na kwamba wanaendelea kujenga vituo ili kuwa na cha magari ya dizeli.

Alifafanua kuwa mifumo ina tofauti kubwa na kwa petroli kwenda gesi ni rahisi kuliko yanayotumia dizeli, lakini kwa kushirikiana na sekta binafsi vitawekwa vituo hivyo ili kukidhi mahitaji yaliyopo.

# TANGAZO

## NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD,JAMOK INVESTMENT LTD,MCHINGA AUCTION MART,GADAU AUCTION MART,AMI AUCTION MART, IGALULA AUCTION MART,BAHARI AUCTION MART, ADILI AUCTION MART,KOTI BROTHERS CO. LTD,PROPERTY MASTER LTD,MULTILINK AGENCY LTD,TWINS AUCTIONS MART, BID CITY AUCTION,JALAS AUCTION MART,HOLLYNESS COMPANY LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| UKONGA | WAWA COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.KND/KGG/KATI/214 KIGOGO KATI 2. NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOPO KINZUDI GOBA | 1.SALUM JUMA MARWA 2.SALUMU JUMA NYANDOTO | 1.KIGOGO KATI 2.KINZUDI GOBA | 08/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | NEZAK INVESTMENT LTD | NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1019002 KIWANJA NAMBA P23439 KIFURU-KINYEREZI | ZACHARIA ANTHONY KAPAMA | KIFURU KINYEREZI-ILALA | 08/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KARIAKOO | MBM MOTORCYCLE SPARES | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NAMBA 101, KITALU "47", HATI NAMBA 52425 | PETER SIMON MSANZYA | KIJITONYAMA -DAR ES SALAAM | 12/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | PETER JAPHET CHAMBA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK013453 | KELVIN DAVID CHAMBA | YOMBO VITUKA SIGARA TEMEKE | 11/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 08/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | TUNDUMA | 08/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | KITETE-MBEYA | 08/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 11/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | FRENK SAMSON LEMAU | SHEWA-MBEYA | 12/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | IPYANA TIGER JUNIOR | NYUMBA | IPYANA TIGER JUNIOR | ILEMI | 12/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | HELENA ANTONY HALENGO | NYUMBA | MARIA ANTHONI SKAWEWE | ILEMI | 13/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KARIAKOO | LAMECK JOHN RUGIGA | NYUMBA | LAMECK JOHN RUGIGA | KIBAMBA MBEZI | 13/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | LATIFA MOSHI MLANZI | NYUMBA | SALUMU OMARI AMIRI | MWANDEGE - MKURANGA | 08/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | OSCAR ELIAMINI CHUWA | NYUMBA | FLORA ELIAMINI CHUWA | MBAGALA KIZUIANI | 11/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | SULTAN MSHINDO KATUNDU | NYUMBA | SULTANI M.KATUNDU | KIMANZICHANA | 12/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | VENANT ERNEST THOMAS | NYUMBA | VENANT ERNEST THOMAS | DONDWE -MKURANGA | 14/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | TRAZIAS BERNARD ISHENGOMA | NYUMBA | TRAZIAS BERNARD ISHENGOMA | MBAGALA MWANAMTOTI | 14/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | HASSAN NURDIN MPATE | NYUMBA | NURDIN HASSAN OMARY | CHIKICHINI CHARAMBE | 08/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HOSEA MARCO OOKO | NYUMBA | KIBADENI J. NYATIENO | ZAVARA -ILALA | 13/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | DAUDI JAKAMUGAH MAKOSIGAH | NYUMBA | KIBADENI J. NYATIENO | ZAVARA -ILALA | 13/11/2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | ATUPELE LABAN MWAIJIBE | NYUMBA | DR. ATUPELE LABAN MWAIJIBE | KIPUNGUNI | 17/11/2024 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | FELIX BIRCKMAS ALOYS | NYUMBA | KASSIAN ANTHON NINDI | TABATA KISUKULU | 17/11/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ILALA | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK033735 | DAVID ABEL MLAU | CHARAMBE -MBAGALA | 11/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | NELSON JUDICA KIMARO | NYUMBA (2) | 1.NELSON JUDICA KIMARO 2.ERICK ISHENGOMA BILIKWIJA | 1.KIMARA BONYOKWA 2.MABIBO | 14/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | JESCA PETER SHIRIMA | NYUMBA | JESCA PETER SHIRIMA | MJOHORONI MOSHI | 13/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | CHEGE REUBEN OGILLO | NYUMBA | CHEGE REUBEN OGILLO | MSARANGA MOSHI | 13/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | MWAJABU AHMEDI KIBWANA | NYUMBA | MWAJABU AHMEDI KIBWANA | BOMANG'OMBE HAI | 12/11/2024 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | JUMA SELEMANI MNDEME | NYUMBA | JUMA SELEMANI MNDEME | MWANGA | 09/11//2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | PLUKERIA MARTIN MANINGI | NYUMBA | PLUKERIA MARTIN MANINGI | KIBOSHO -KOMBO | 11/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | SAMIJI ATHUMANI KIMBWEREZA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | SAMIJI ATHUMANI KIMBWEREZA | MAKANYA SAME | 13/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | MOSES YARED CRY | NYUMBA | MOSES YARED CRY | ZAVARA BUYUNI | 08/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | ANNA IVAN SUTILA | NYUMBA | ANNA IVAN SUTILA | MBEZI JUU | 15/11//2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | RAYMOND SAMSON LAISER | NYUMBA | RAYMOND SAMSON LAISER | KIHARAKA BAGAMOYO | 15/11/2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | MTIBU FISH ENTERPRISES | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.DSMT1026616, BONYOKWA | HAMISA BAUSI ABUU | KIMARA BONYOKWA | 15/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ILALA | LAURENCIA ROBERT KIROBI | NYUMBA | LAURENCIA ROBERT KIROBI | KIBADA | 08/11//2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ILALA | DANIEL FADHIL MINJA | NYUMBA | DANIEL FADHIL MINJA | MAJOHE | 15/11//2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ILALA | RENIFRIDA CHARLES MGUDE | NYUMBA | RENIFRIDA CHARLES MGUDE | SARANGA | 15/11//2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARIA JOHN PETRO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JOHN PETRO KALISA | KILOLELI 'B' - MWANZA | 12/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO0 |
| MWANZA | JOSEPH KIGONGO IBAMBASI | NYUMBA | JOSEPH KIGONGO IBAMBASI | NYAKATO MWANZA | 14/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MASHAKA CHARLES BULUBA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | MASHAKA CHARLES BULUBA | NYASAKA | 12/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | GRACE ADONIAS MTEGO | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.22 KITALU 'N' HATI NA.4870 | BLASIUS SWAI KAGINA | BUNDA | 13/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | ABAS HAMAD ISSA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PETER NDULU MAHARAGE | MISUNGWI | 15/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JAMES JACOB KALULEMA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JAMES JACOB KALULEMA | NYANGURUGURU MAHINA | 11/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | KITU MAYALA MANGA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | KITU MAYALA MANGA | KISESA | 14/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MAWAZO JOHN SIMON | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | EDWIN GASPARY NYAMTABA | KANYERERE | 14/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JOSIAH JOHN JOACHIM | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JOSIAH JOHN JOACHIM | KISESA MWANZA | 14/11/204 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | CHACHA ITEMBE NYAMAISA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | SHABANI S. BULILO | NYAMHONGOLO | 12/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | HELENA IGNATUS NYAKARASHI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | GEORGE SILIVESTER ADOGO | NYAMADOKE BUSWERU | 17/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MAGWE EMMAUEL WAMBURA | VIWANJA (3) VYENYE HATI MILIKI | MAGWE EMMANUEL WAMBURA | ILALILA-MWANZA | 17/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | IMORY FREDRICK IMORY | NYUMBA,YENYE HATI NA.99386 | IMORY FREDRICK IMORY | BUKAGA MWANZA | 21/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | DENIS DEOGRATIAS NSHEKANABO | NYUMBA YENYE HATI NA.103641,KIWANJ | DANIEL MABULA KAHUNGWA | NYAMANORO ILEMEALA | 21/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | ALOYCE ALOYCE KIMARO | NYUMBA | YAHAYA HUSSEIN ATHUMAN | PASIANSI MWANZA | 17/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | HAPPINESS NYANDA MAYALA | NYUMBA YENYE HATI NA. 99009, KIWANJA NA."9" KITALU " F" | SAIDI NYANDA MAYALA | IGOMA MWANZA | 17/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | ABDALLAH AHMAD MUHIDINI | NYUMBA | ABDALLAH AHMAD MUHIDINI | TEGETA 'A' - GOBA | 12/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | MARTHA ONESPHORY NCHIMBI | NYUMBA | MARTHA ONESPHORY NCHIMBI | MGEULE JUU-CHANIKA | 13/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | BRILUCK SECRETARIAL SERVICE | NYUMBA | ADOLF ANSELM MNG'ANYA | MBEZI MSAKUZI | 08/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | DEVOTA JOHN KATINDASA | NYUMBA | MASOUD HAMAD SEIF | KICHANGANI- MAJOHE | 12/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | MHINA JOSEPH KWELLA | NYUMBA | MHINA JOSEPH KWELLA | PUGU | 15/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | STEWART EDSON MWANGALABA | SHAMBA | STEWART EDSON MWANGALABA | MKURANGA | 18/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | MICHAEL LAURENTI MPOGOLE | NYUMBA | MICHAEL LAURENTI MPOGOLE | MBEZI KIBAMBA | 14/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | AMRI BAKARI MAKANYA | NYUMBA | MWANAHAMISI KASSIM YUSUPH | KITUNDA | 13/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | JACQUELINE LAMECK KIBOGA | NYUMBA | SABATO DAVID OKUKU | MIKWAMBE- TOANGOMA | 15/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | CESILIA SAMWELY KWEKA | NYUMBA | LEONARD JACOB NUBWA | MBAGALA- MISSION | 19/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | MTUMWA SALUM HAMAD | NYUMBA | MATONGO NKWABI NSWAGA | PUGU KINYAMWEZI | 18/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | ANDREW SAMSON GESURURA | NYUMBA | ANDREW SAMSON GESURURA | BASIHAYA-BOKO | 18/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | MUSSA INANO CHACHA | NYUMBA | HABIBU MUSSA MACHOROKO | MBAGALA | 19/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | SAINT PIO DAY CARE CENTRE | NYUMBA | JESCA JAMES SUGWEJO | MABWEPANDE | 18/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | MWANAHAMIS VITUS FRANK | NYUMBA | HADIJA MOHAMED CHANDE | MSINGWA-MSIGANI | 08/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | SELEMANI HEMED SELEMANI | NYUMBA | SELEMANI HEMED SELEMANI | MBAGALA KIBONDE MAJI | 12/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | SHAMSI FADHILI MASISA | NYUMBA | SAAD ADAM MDOE | KINYAMWEZI KATA YA PUGU | 14/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | WINNIE ADOLE RWIZA | NYUMBA | WINNIE ADOLE RWIZA | KANGA-KINYEREZI | 11/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | SALVATORY MODESTI NGOWI | NYUMBA | SALVATORY MODESTI NGOWI | KIPUNGUNI 'B'-KITUNDA | 12/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | KURUTHUMU ALLY HUSSEIN | NYUMBA | FUAD JAFARI ABDALLAH BIN SHMLAN | PEMBA MNAZI -KIGAMBONI | 13/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | FREDRICK ALLY SANGA | NYUMBA | FREDRICK ALLY SANGA | KIVULE-ILALA | 12/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | FATUMA MSOMA KIULA | NYUMBA | AMIRI OMARI LUPATU | MAJOHE-KICHANGANI | 18/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | JIMMY MLAGANO CHANGAS | NYUMBA | JIMMY MLAGANO CHANGAS | BUNJU "B" | 15/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | GIDION YORAM ISACK | NYUMBA | GIDION YORAM ISACK | CHANIKA-YONGWE | 14/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | LEOKADIA SOSTHENES MPONZI | NYUMBA | LEOKADIA SOSTHENES MPONZI | MACHIMBO - KIPUNGUNI | 18/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | GLADNESS PETER BOLOHO | NYUMBA | GLADNESS PETER BOLOHO | BOMBAMBILI KIVULE | 15/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | ONESMO PETER MASIMA | NYUMBA | ONESMO PETER MASIMA | UKONGA MAZIZINI | 15/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | JULIUS RYOBA DANIEL | NYUMBA | JULIUS RYOBA DANIEL | KITUNDA- MZINGA, ILALA | 14/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | MAX AYUBU MBONYE | NYUMBA | MAX AYUBU MBONYE | YONGWE-CHANIKA | 18/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | ROBERT CHACHA NYAMBARI | NYUMBA | ROBERT CHACHA NYAMBARI | KITUNDA MTAA WA KINYANTIRA | 11/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | ABDALLAH SEIF MATIMBWA | NYUMBA | ABDALLAH SEIF MATIMBWA | VIWEGE-MAJOHE, ILALA | 11/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | AMA ABDALLAH KIPENDE | NYUMBA | AMA ABDALLAH KIPENDE | KIBAONI KISARAWE - PWANI | 08/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | CHRISTOPHER CHACHA MAGWE | NYUMBA (2) | 1. CHRISTOPHER CHACHA MAGWE 2. EUNICE ELIGUARD MMARI | 1.CHINANGALI 2.NALA - DODOMA | 14/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | IVAN MAWAZO JACKSON | NYUMBA | IVAN MAWAZO JACKSON | MPUNGUZI -DODOMA | 13/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| HEAD OFFICE | ANNANEEMA DANIEL RITTE | KIWANJA | ANNANEEMA DANIEL RITTE | SEGU CHINI, KATA YA NALA - DODOMA | 12/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| HEAD OFFICE | ADAM DAVID KESSY | KIWANJA | ADAM DAVID KESSY | KISOPWA KWEMBE | 08/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ARUSHA | OLIVER STANLEY MNDEME | NYUMBA | OLIVER STANLEY MNDEME | KIMANDOLU - ARUSHA | 11/10/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | HP PLANNERS & EVENTS MANAGEMENT LTD | NYUMBA (2) | 1.JAMES NDASKOI NNKO 2.DAPHROSER ABEID HAMZA | 1.TEGETA 2.KIGAMBONI | 15/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MAIN | TECHNO COMBINE CONSTRUCTION LTD | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PEREZ SOLOMON JACOB | KIMARA MAVURUNZA | 23/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MAIN | JAR TECHNOLOGIES | NYUMBA | JULIANA EPIMARK MBWANI | UNGINDONI KIBAHA | 21/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | FAISAL SALUM HASSAN | GARI T396 DJR HINO RAINBOW | FAISAL SALUM HASSAN | TEMEKE | 15/11/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | LITTLEWOOD NURSERY AND PRIMARY SCHO | TOYOTA HIACE T362DMF | MARWA NTAGIRA NTAGIRA | KINYEREZI | 22/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | JAMAL SWALEHE RASHID | NYUMBA | JAMAL SWALEHE RASHID | NALA-DODOMA | 21/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | ROBERT NASSON MAKAPI | NYUMBA | ROBERT NASSON MAKAPI | HOMBOLO BWAWANI - DODOMA | 22/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | KEVINNI KORNEL MSAGAMASI | NYUMBA | KEVINNI KORNEL MSAGAMASI | NZUGUNI 'A' DODOMA | 22/11/2024 SAA 5:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | KOLE JOSEPH SAINI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | KOLE JOSEPH SAINI | BOMBAMBILI ILALA DAR ES SALAAM | 15/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | SLIDE VISUALS LIMITED | GARI TOYOTA LANDCRUISER T127 EAC | SLIDE VISUALS LIMITED | MWANANYAMALA KOMAKOMA | 22/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | JUMBE MHINA SALUM | NYUMBA | JUMBE MHINA SALUM | MKENGE-VIKAWE | 13/11/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | SYLIVESTER APOLINARY MBOYA | NYUMBA (2) | 1. SYLIVESTER APOLINARY MBOYA 2.KIMANG | 1.MBEZI MSUMI 2.ZOMBOKO CHARAMBE | 15/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | MPOKI BROWN MWAIPASI | NYUMBA | MPOKI BROWN MWAIPASI | KILUVYA | 22/11/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | OSCAR JOSSEY MUNIS | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | VERAELI ELIYA KOMBE | MWANANYAMALA -KINONDONI | 13/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MTONDI SIAGI KICHELE | NYUMBA | KURUTHUMU ABDALLAH NYAMKO | NYAKATO -MWANZA | 14/11/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0714939933/0759648448/0715868000/0714208208/0759648448/0755337777/0715363537/0713306054**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uchaguzi Serikali za Mitaa wachaguliwe wanaowajibika

**UCHAGUZI** wa serikali za mitaa unatarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu na uchaguzi huu utumike kuchagua viongozi wanaowajibika kwa wananchi kwenye mitaa yao.

Wananchi wamechoka kuona viongozi wanaowachagua wakikaa ofisini kusubiri kugonga mihuri ya barua, wakati wakipelekewa kero, hawazishughulikii.

Kero kubwa kwenye mitaa ni uchakavu wa miundombinu ya barabara, ulinzi na uzoaji taka. Ingawa kuna kero nyingine zinazogusa familia, lakini haya matatu yanaongoza kwa kulalamikiwa. Viongozi wengine wanapoona wananchi wakijichanga kushughulikia kero hizo wananuna wakifikiri kwamba wanataka kunyang'anywa nafasi zao. Huu sio uongozi bali ni ubinafsi wa kupenda madaraka.

Uchaguzi huu pia uwe chachu ya kuwaibua wanawake wengi kushiriki kuwania nafasi za uongozi. Wakati wa wanawake kutumika kama wapiga kampeni na kuwa ngazi za kupandishia wenzao kugombea nafasi hizo umepitwa.

Ni haki ya kila mmoja kushiriki kupigakura na kuchaguliwa hivyo wanatakiwa kuamka na kujitokeza kwa wingi.

Huu ni wakati wa kuonesha kuwa wanawake wanaweza kupambana na kushinda kwenye chaguzi kutokana na watakavyoweza kujieleza na kumwaga sera zao.

Kukatishwa tamaa kuwe mwiko kwao na wasikubali kuwekewa vikwazo vya aina yoyote ile.

Wengine wanakosa ujasiri wa kuthubutu baada ya kuona wenzao wanavyopata misukosuko ikiwamo kudhalilishwa na kutukanwa kwenye majukwaa. Miongoni mwa sababu zinazowadhoofisha wanawake wengi kujitokeza kuwania nafasi iwe kwenye siasa au taasisi ni kuombwa rushwa ya ngono.

Hii ni vita kubwa na inapaswa kukomeshwa na wanawake wenyewe kwa kujitambua na kutokubali kudhalilishwa kwa namna yoyote ile. Kwenye nafasi za kisiasa, wanawake wengi hulalamika kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji kwa kuitwa majina ya ajabu ajabu ili tu wakatishwe tamaa.

Kwa wanawake walio kwenye ndoa wanakuwa kwenye mtihani mkubwa baada ya wenza wao kusikia yanayofanyika kwenye mchakato wa kuwania nafasi hizo na kuamua kuwakataza ili kuepuka kashfa. Suala hili linahitaji kukemewa na pia elimu ya kutosha kuanzia mijini na vijijini ili wanawake wengi waelimike na kujitokeza kuwania nafasi.

Vyama vya siasa, wanaharakati wa haki za binadamu mna kazi kubwa ya kutoa elimu kupiga vita jambo hilo.

Kwa kudhoofisha wanawake kujitokeza kuwania nafasi za uongozi, kunaweza kukapoteza ari yao ya kuonesha vipaji vyao vya uongozi. Na katika maeneo mengi ya kazi imeshuhudiwa kuwa wanawake wanapopewa uongozi wanafanya vizuri na hata suala la rushwa ya ngono huwezi kulisikia.

Mapambano ya rushwa ya ngono ni lazima yawe makubwa ili kukomesha hali hiyo kabisa.

Aidha, wanawake wajitahidi kuhamasishana wajitokeze kugombea nafasi mbalimbali wasibakie kuwa wapiga kura.

Katiba inaruhusu kugombea, kupiga kura na kupigiwa, lakini bado hawajitokezi kwa hofu ya udhalilishaji.

"Vikwazo vipo vingi vinavyowafanya wanawake washindwe kujitokeza kugombea, sababu moja wapo hatuna uthubutu, pili, elimu ya uraia haiwafikii kinamama nje ya miji, juhudi zifanyike wafikiwe. Rushwa ya ngono ni kikwazo, waume zetu wakisikia unataka kugombea wanakukataza kama haujaolewa wazazi wanakukataza kugombea," anasema aliyewahi kuwa waziri wa zamani Shamim Khan.

Mwanamke akitaka kugombea nafasi yoyote anapaswa kukataa rushwa ya ngono na akiwa na heshima yake hakuna atakayemfuata. Pia, ni muhimu wakajua kanuni na vyama vya siasa vifanye bidii kupeleka kanuni hizo hadi ngazi ya chini ndipo watapatikana wanawake wengi.

Kuna nafasi za viti maalum vya udiwani na ubunge, ambazo zimependekezwa na wadau wa siasa ziwe na ukomo wa miaka kumi ili kutoa nafasi kwa wanawake wengine kuziwania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# Staili hii 'kuchimba dawa' kinamama safarini, hatutendewi haki jamani!

**KWA** yeyote mwenyeji wa kusafiri mbali tena kwa basi, anafahamu vyema utaratibu wa abiria kupewa fursa ya 'kwenda kuchimba dawa.'

Hilo sio la jana au juzi, bali lina muda mrefu sana kihistoria na tukio hilo hufanyika kuwapa watu faragha ya kwenda kujisaidia zaidi katika pori teule au mahali penye huduma, japo zaidi hufanyika porini.

Ni utaratibu unaoangukia katika sura ya utamaduni husika, ndani ya pori teule hilo ambako madereva na makondakta wao ni wenyeji hasa, huwatenganisha katika jiografia ya mahali hapo kijinsia wajisitiri.

Hapo ndipo kinapokuja kilio kingine cha jinsia moja, kinamama wanapojisaidia, kulingana na uhalisia wa faragha hiyo wanajikuta katika mazingira ya kudhalilika.

Mfano hai nauelekeza kwa mabasi yanayosafiri kuelekea mikoa ya Kusini mwa nchi, kutoka Dar es Salaam. kunashuhudiwa kuanzia ngazi ya mkoa jirani Pwani, upande wake wa Kusini katika wilaya za Kibiti na Rufiji, kisha kuelekea mikoa ya Lindi na Mtwara, hadi Mtwara.

Kumekuwapo mabasi yanayoelekea njia hizo kwenda mikoa ya Kusini, yanayoanza safari zake kutoka Temeke, hadi Mbagala, Dar es Salaam, pale yanapofika maeneo ya Mkuranga mkoani Pwani, huingia katika vituo vya mafuta na kupaki.

Hapo ndipo zinarejea salamu za wasimamizi wake kwa abiria wakitakiwa 'wakachimbe dawa', wanapewa muda wa dakika tano.

Wapo wanaoshuka 'kuchimba dawa' kwa wakati sahihi na wanarudi kuendelea na safari kama ilivyo ratiba waliyopewa.

Hao abiria walioshuka katika kituo hicho 'wanachimba dawa' na kunawa mikono kwa huduma ya maji na sabuni iliyoko mahali hapo kwa wakati.

Hata hivyo, nikiri hiyo ni kwa baadhi ya mabasi na sio kwa yote. Yapo ambayo yananishangaza, mabasi hayasimami mahali hapo katika maeneo sahihi, ambayo abiria 'huchimba dawa' na badala yake wanapaki gari barabarani, wakiwaambia abiria washuke kuchimba dawa kwa dakika hizo tano zilizo zoeleka kwa utaratibu wa mabasi mengi.

**Kitendo cha kuwachimbisha dawa abiria hawa kinamama kweupe barabarani, mnakuwa hamjawatendea haki hata kidogo! Ni bahati mbaya inakuwa kama tabia, kwani sio matendo ya basi moja au mawili pekee.**

Ukiangalia gari linapaki barabarani, halafu abiria wanaambiwa wachimbe dawa kwa muda wa dakika tano, huku huduma inayotakiwa haijakaa sawa.

Kwa kweli, uchimbaji dawa huo unawadhalilisha wanawake, kwa sababu wanawake wanalazimika kukimbia ovyo vichakani kupata faragha ya huduma za 'kuchimba dawa.'

Hapo tena, magari kuna mengine unakuta yanasimama barabarani na kuwaambia abiria wa kike wazunguke nyuma ya gari ili 'wachimbe dawa.' Ukiangalia hao wahusika wanaosema abiria wa kike wazunguke nyuma ya gari, tunajiuliza wana maana gani?

Ni kwa maana huko yanapita magari mengine yanayosafiri. Kwa kweli mwanamke anakuwa hajatendewa haki.

Msingi wake unatakiwa utaratibu ufanywe, kama magari mengine yanavyofanya kwa kupelekwa abiria katika migahawa au vituo vya mafuta, ili watu 'wachimbe dawa' wakiwa katika mzingira huru.

Kitendo cha kuwachimbisha dawa abiria hawa kinamama kweupe barabarani, mnakuwa hamjawatendea haki hata kidogo! Ni bahati mbaya inakuwa kama tabia, kwani sio matendo ya basi moja au mawili pekee. Ikumbukwe kuwa, wanawake hawapo sawa na wanaume, kwa kuwa mwanaume anaweza kusimama na akafanya jambo lake, lakini inakuwa tofauti kwa mwanamke.

Hivyo inatakiwa suala la 'kuchimba dawa' liwajali wanawake katika uhalisia wao na sio kuwadhalilisha kwa kuwaambia wachimbe dawa maporini au barabarani. Ni hatua inayochukua hatari, wakati majibu mbadala wake yapo bayana.

Niseme kama vile kuna mamlaka mengi tu yanayosimamia tafsiri za usalama wa barabarani wakiwamo Polisi wa Usalama wa Barabarani na LATRA, kuhakikisha nafasi hiyo ya kijinsia inaishi katika usalama, ambayo tafsiri yake inafikia hata utetezi wa nafsi yake.

HABARI KITAIFA

## Utafiti: Wananchi wanashindwa kumudu gharama za nishati safi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

UTAFITI uliofanywa na shirika lisilo la kiserikali la Relief to Development Society (REDESO), umebaini asilimia 80 ya wakazi wa kata ya Mkuza, Halmashauri ya Mji wa Kibaha wanashindwa kuhama kutoka kutumia nishati chafu kwenda nishati safi kutokana na uwezo mdogo kifedha.

Uwezo huo mdogo kwa baadhi ya wananchi wa kata hiyo unadaiwa kuwa sababu ya kuendelea kutumia kuni na mkaa kupikia badala ya gesi na nishati ya umeme.

Hayo yalibainishwa juzi mjini Kibaha na Mtendaji Mkuu wa shirika hilo, Abeid Kasaizi wakati wa ufunguzi wa mradi wa majaribio wa utoaji elimu kwa wanawake na vijana kuhusiana na matumizi ya nishati safi na majiko banifu.

Kasaizi alisema takwimu hizo zimepatikana baada ya kufanya mahojiano na baadhi ya wakazi wa kata hiyo ya Mkuza, wakijumuisha mama lishe, baba lishe na bodaboda kuhusiana na kikwazo cha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwenye shughuli zao.


Mtendaji Mkuu huyo alisema asilimia 62 ya wananchi waliohojiwa walieleza kwamba hawana uelewa wa nishati safi ya kupikia, jambo lililotoa msukumo kwa shirika hilo kufanya mafunzo.

Alieleza kwamba katika awamu ya kwanza, mafunzo hayo yatawafikia walengwa 250 na baadaye wengine 50 watafanya kwa nadharia huku malengo yakiwa kushirikiana na vyuo vya ufundi ili mafunzo yafike nchini nzima.

"Mradi huu wa majaribio unalenga kutaka kujua tatizo linalowakabili baadhi ya wananchi kutumia nishati safi pamoja na kuwapo kwa jitihada nyingi zinazofanywa na serikali kuondoka kwenye matumizi ya nishati chafu," alisema.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Demetria Dionzi, mkazi wa Kwamatiasi, mjini Kibaha, alisema serikali inatakiwa kuangalia namna ya kuwajali wanawake, mamalishe wanaotumia gesi, ipatikane kwa urahisi na gharama nafuu.

Naye Castro Geassy alisema nishati gesi kwenye vyombo vya moto ikipatikana kwa urahisi, itakawasaidia kupunguza gharama za mafuta wanayotumia hivi sasa.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe akijibu maswali ya baadhi ya Wabunge, Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yashtuka walimu wengi kukimbilia mijini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewaagiza wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kufanya msawazo wa walimu ili maeneo ya vijijini yasikose walimu kutokana na wengi wao kukimbilia mijini.

Agizo hilo lilitolewa jana na Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Zainab Katimba alipojibu maswali ya wabunge waliohoji mkakati wa serikali wa kutatua changamoto ya upungufu wa walimu katika shule za msingi nchini.

Miongoni mwa wabunge hao ni wa Tabora Mjini (CCM), Adamson Mwakasaka ambaye alihoji mkakati wa serikali wa kumaliza upungufu mkubwa wa walimu shule za msingi nchini.

"Katika Jimbo la Tabora Mjini lenye kata 29, kuna upungufu wa walimu hasa maeneo ya pembezoni. Je, serikali ina mpango gani wa kupeleka walimu maeneo hayo?" alihoji.

Alisema walimu wengi hawapendi kwenda vijijini na wamejazana mijini hasa kwenye shule za msingi na kuhoji mkakati wa serikali wa kuhakikisha walimu wanakaa vijijini na kuacha tabia ya kukimbilia mijini.

Mbunge wa Moshi Vijijini (CCM), Prof. Patrick Ndakidemi, alisema shule nyingi za msingi katika jimbo hilo zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa walimu na kuna baadhi ya shule zina walimu watatu, akihoji mpango wa serikali kupata walimu ili kuondokana na tatizo hilo.

Mbunge wa Tarime Vijijini (CCM), Mwita Waitara alihoji serikali itahakikisha vipi wale walimu ambao wamehitimu muda mrefu, wanapata ajira kupitia utaratibu wa usaili kwenye ajira zilizotangazwa hivi karibuni.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Katimba alisema serikali inatambua kuna tatizo la walimu kupenda kukaa mijini na kuwaagiza wakurugenzi kwa kuzingatia bajeti wahakikishe wanafanya msawazo wa walimu ili kuweka uwiano ulio mzuri na kuondoa mrundikano wa walimu kwenye baadhi ya maeneo huku mengine yakiwa na upungufu.

Alisema serikali inaendelea kutekeleza hatua tofauti tofauti za kuboresha mazingira ya kazi kwa walimu kwa kuhakikisha huduma zote za msingi zinapatikana vijijini ili walimu wafanye kazi na kuacha kukimbilia mijini.

Aliwahakikishia wabunge kuwa watapata mgawo wa walimu kwenye maeneo yenye upungufu kwa kuwa tayari serikali imeshatangaza kuajiri walimu.

Awali, alibainisha kuwa serikali imekuwa ikiajiri walimu wa shule za msingi kila mwaka kulingana na upatikanaji fedha na kwa kipindi cha mwaka 2020/21 hadi 2022/23, serikali iliajiri walimu 16,598 wa shule za msingi.

Alisema kuwa Julai 20, 2024, serikali ilitangaza ajira za walimu 11,015 wakijumuisha walimu 3,370 wa shule za msingi na mchakato wa ajira ukikamilika watapangiwa vituo vya kazi.

Hata hivyo, akijibu kuhusu utaratibu wa ajira kuzingatia walimu waliohitimu muda mrefu, alisema serikali ina utaratibu wake kulingana na vigezo ilivyojiwekea na kwamba imepokea mawazo ya Mbunge Waitara.

## KABWELA

Na Fadhil Mohammed



UCHAGUZI WA MITAA

# Serikali yaahidi utulivu siku ya upigaji kura

**Na Moses Ng'wat,** TUNDUMA

KATIBU Tawala wa Wilaya ya Momba, Frank Nkinda, amesema kuwa serikali wilayani humo imejipanga vilivyo kuhakikisha siku ya uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika Novemba 27, mwaka huu, hali ya usalama, amani na utulivu vinatawala.

Alibainisha hayo wakati akitoa salamu za serikali alipomwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Momba, Elias Mwandobo, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji Tunduma kilichoketi kwa lengo la kupitia taarifa za utekelezaji kwa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/25.

"Kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya, naomba nilihakikishie Baraza lako nikiwa na kamati ya kuu (Kamati ya Ulinzi na Usalama) tumejipanga vilivyo kuhakikisha kuwa siku ya uchaguzi amani na utulivu vinatawala," alisema.

Aidha, Nkinda aliwahimiza madiwani na watumishi wa halmashauri hiyo, viongozi mbalimbali wa kisiasa na madhehebu ya dini kuendelea kuhamasisha na kuwapa elimu wananchi waliojiandikisha kwa ajili ya kupiga kura kujitokeza kwa wingi kwenda kupiga kura Novemba 27, mwaka huu.

Awali, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma, Mwanaisham Nassor, alivitaka vyama vya siasa katika halmashauri hiyo kuzingatia kanuni za uchaguzi zilizowekwa ili kudumisha hali ya amani na utulivu katika kipindi chote cha mchakato wa uchaguzi huo.

Mwanaisha alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha kunakuwa na uchaguzi huru na wa haki, huku akitoa rai kwa vyama vya siasa kufanya kampeni za kistaarabu bila kuleta taharuki.

Akifunga kikao hicho, Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Ayoub Mlimba, aliwakumbusha wananchi kushiriki uchaguzi kwa utulivu huku wakitambua kuwa baada ya kupiga kura kuna maisha yatapaswa kuendelea.




Mkurugenzi wa Kitengo cha Ajira kutoka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu, Joseph Nganga akizungumza wakati wa mdahalo wa kujadili uhamiaji wa wafanyakazi unaolenga kukuza ajira salama zenye staha kwa wahamiaji wa Kitanzania na kupunguza vihatarishi mbalimbali, uliofanyika jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Akaunti ya pamoja Muungano kufunguliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imelihakikishia Bunge kuwa akaunti ya pamoja ya Muungano itafunguliwa baada ya kukamilisha mashauriano yanayoendelea kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar.

Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha, Hamad Hassan Chande, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Chonga (ACT Wazalendo), Salum Mohamed Shaafi.

Shaafi alihoji kama akaunti hiyo imefunguliwa.

Naibu Waziri Chande alisema serikali hizo mbili zinaendelea na mashauriano ya mapendekezo yaliyowasilishwa na Tume ya Pamoja ya Fedha kuhusu utaratibu wa kudumu wa kuchangia matumizi na kugawana mapato ya Muungano.

"Uamuzi wa pamoja utakapofikiwa na pande mbili za Muungano, ndiyo utakaowezesha kufunguliwa kwa akaunti ya fedha ya pamoja," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alihoji kutokana na kuchelewesha kuundwa kwa akaunti ya pamoja ya serikali, serikali haioni nia njema ya ufunguaji wa akaunti hiyo.

"Ufunguaji wa akaunti hii ya pamoja ni takwa la kikatiba na sio la kimashauriano, nataka kufahamu ni sababu zipi zilizosababisha mashauriano hayo hadi leo kutokukamilika," alihoji.

Akijibu, alisema serikali ina nia njema ya kufungua akaunti hiyo na kwamba kulikuwa na kero za Muungano 25 hadi sasa 21 zimefanyiwa kazi na zilizobaki serikali ipo kwenye mchakato wa kuzitatua.

# Mkemia awaonya watumishi kemikali ya sodium sianidi

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imetoa tahadhari kwa wananchi na wachimbaji madini kuhusu kemikali ya sodium sianidi, ikisema ni hatari kiafya endapo ikikiukwa masharti ya matumizi na kinga.

Imesema kemikali hiyo ni mojawapo ya sumu kali zaidi duniani, kutokana na uwezo wake wa kusababisha kifo haraka kwa sababu huweza kuchanganyika kwa wepesi na maji na vyuma.

Mkemia kutoka ofisi hiyo, Derick Masako alitoa tahadhari hiyo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa elimu kwa wananchi namna ya kujikinga na kemikali hiyo pindi gari la usafirishaji likipata ajali au kumwagika barabarani.

"Hewa ya sumu inayoitwa haidrojeni sianidi inaua haraka sana. Hii kemikali inatumika kwenye migodi kukamatia dhahabu lakini ikimwagika barabarani hewa yake ni hatari sana, ndiyo maana leo tupo hapa kuwapa elimu wananchi namna ya kujikinga. Wakiona kemikali hii imemwagika wakae mita 100 umbali na eneo la tukio," alisema Masako.

Alisema kemikali hiyo iliingia nchini mwaka 1998, kwamba Ofisi ya Mkemia Mkuu imekuwa ikitoa elimu na kuwasajili waagizaji, wanaohifadhi na watumiaji.

"Ni kemikali ambayo inatumika katika uchimbaji dhahabu, kutokana na uwezo wake wa kuyeyusha dhahabu kwa umakini mkubwa kutoka kwenye matope au mchanganyiko mwingine wa maji. Lakini ikikiukwa masharti ina madhara makubwa sana," alisema.

Kuhusu athari kwa wafanyakazi kwenye migodi, Masako alisema: "Migodi yote tumeisajili kama sehemu ya watunzaji na watumiaji wa kemikali. Kwenye migodi madhara siyo makubwa kwa sababu mashine ndizo zinazofanya kazi. Lakini kwa wananchi tumelazimika kuwapa elimu kwa sababu wao wakiona gari lolote limepata ajali wanakimbilia."

Ofisa kutoka kampuni inayohusika na usafirishaji wa kemikali hiyo ya Taifa Trasport, Bestina Kitinya alisema lengo la kutoa elimu hiyo ni kuwapa uelewa wananchi kuhusu athari na namna ya kujikinga na kemikali hiyo.

Alisema wananchi wanapoona gari lolote lililobeba kemikali limepata ajali wanapaswa kutolisogelea bali wakae umbali wa mita 100.

Alisema pia wanapaswa kutoa taarifa haraka katika vyombo vya ulinzi na usalama au uokoaji au kupiga simu namba 112.

Bestina alisema: "Kila mwaka tunatoa elimu hii ya kujikinga na athari za kemikali. Leo tupo hapa Dar es Salaam, kesho tutakuwa Pwani na siku zijazo tutakuwa Singida na mikoa mingine. Lengo ni kupunguza majanga yatokanayo na ajali za kemikali."

Kadhalika, alisema usafirishaji wa kemikali ya sianidi umezingatia sheria na taratibu zote, ikiwamo kuchukua tahadhari kwa magari yanayotumika kusafirisha.



# Watumishi TFS waliokaimu vyeo waula

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) imeagizwa kuwathibitisha watumishi wenye sifa baada ya kukaimu nafasi hizo kwa muda mrefu ili kuongeza ufanisi na tija katika utendaji wa kazi.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana wakati akifungua mkutano wa tatu wa mwaka wa viongozi na makamanda wa hifadhi hiyo wenye kauli mbiu ya 'TFS 2024, huduma kwa uadilifu'.

"Watu waliokaimu nafasi mbalimbali muda mrefu na zile zilizo wazi hakikisheni zinajazwa ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji kazi," alisema.

Alisema umefika sasa wakati kwa wale wanaokaimu nafasi mbalimbali kuidhinishwa ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi kwa serikali na kusimamia maboresho ya maslahi ya wafanyakazi kwa kuwapandisha vyeo na madaraja.

Chana, alisema ni wakati sasa kwa menejimenti ya TFS kuhakikisha wanaboresha maslahi ya watumishi, kwani imetangaza nafasi za ajira kwa watumishi zaidi ya 265, hivyo wahakikishe wanachagua watumishi bora wanaoendana na kasi ya mabadiliko.

Kuhusu majanga ya moto yanayotokea kwa baadhi ya maeneo ya hifadhi za misitu nchini, alisema endapo wananchi watapewa elimu ya usafishaji mashamba, wataweza kuyahifadhi na kuepuka moto kusambaza kwenye rasilimali hizo wakati wa msimu wa kilimo, kuepuka uingizaji mifugo na kudhibiti uharibu wa mazingira ya hifadhi.

Aliwakumbusha kusimamia viapo vyao vya kazi na kutanguliza weledi wenye mbinu za kijeshi, kuzingatia haki jinai, uzalendo, ari ya ufanyakazi kazi katika kukabiliana na changamoto za uhifadhi na migogoro baina ya wananchi.

Vilevile Chana, aliiagiza mamlaka hiyo kuanza kutumia teknolojia ya kisasa ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kubaini changamoto zinazotokea ndani ya maeneo yao, majanga ya moto badala ya kusubiri kupewa taarifa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri wa TFS, Brigedia Jenerali, Mbaraka Mkeremy, alisema bodi imetatua chagamoto za watumishi na wenye sifa kupandishwa madaraja.

Mkeremy, alisema hadi kufikia Juni mwaka huu, bodi imesimamia ujenzi wa majengo mapya 70, ununuzi wa vitendea kazi na idadi kubwa ya watumishi kupata mafunzo ya kijeshi, huku wengine wakisubiri katika kutimiza ulinzi wa rasilimali za misitu na nyuki.

Alisema bodi hiyo imesimamia maduhuli ya serikali, hadi Juni mwaka huu, imekusanya Sh. bilioni 166 kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2023/24.

Alisisitiza ubunifu kwa kuwa ni muhimu kuhakikikisha mashamba ya miti yanaimarika na kuongeza malighafi ya kutosha katika viwanda zaidi ya 8,002 nchini vinavyotegemea miti.

Kamishna wa Uhifadhi wa TFS, Profesa Dos Santos Silayo, alisema mkutano huo una lengo la kujengeana uwezo, kubadilishana uzoefu wa utendaji kazi, wajibu wa ushirikiano kazini na kuimarisha mifumo ya utendaji.

Mkutano huo umeshirikisha wahifadhi wakuu wa mashamba misitu, wakuu wa divisheni wa Shamba la Taifa la Miti la Sao Hill, Wahifadhi wa Wilaya wa TFS , Wahifadhi wa Misitu ya Asili, Wakuu wa Vituo vya Uzalishaji Mbegu za Miti na Vituo vya Malikale.

## Wakabidhiwa hatimiliki 240 viwanja vya NHC

**Na Allan Isack,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda amekabidhi hatimiliki za ardhi 240 kwa wananchi walionunua viwanja Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) mkoani hapa.

Pinda, amewataka wananchi hao kutambua thamani ya hati hizo na kuzilinda kwa kuwa zina faida kubwa hasa fursa ya kukopa fedha kutoka taasisi za fedha na benki.

"Hati thamani yake ni kubwa sana kwenye maisha yetu ya sasa, nawaomba hata kama unataka kujenga ghorofa 10 hati hii peke yake ni neno kwa wenye mapesa yao, ukienda benki utadhaminiwa na tumetoa hati 240," alisema.

Naibu Waziri huyo aliwataka watumishi wa ardhi kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kutumia lugha nzuri na kuacha kuzua taharuki kwa watu kufuatilia huduma za ardhi katika ofisi zao mara kwa mara.

Alimtaka Mkurugenzi wa NHC mkoani hapa, kuacha kuuza nyumba zilizopo mjini badala yake wajenge majengo yenye uhitaji na maeneo ya mjini.

Meneja wa NHC Kanda ya Kaskazini, Benit Masika, akisoma ripoti ya mradi wa Safari City, alisema upo Burka-Mateves Jiji la Arusha kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari 587 katika mpango kabambe ulioandaliwa mwaka 2014.

Masika, alisema mradi huo una viwanja 1913 kwa ajili ya uendelezaji nyumba za makazi, majengo ya biashara, huduma za jamii ikiwamo shule, vyuo, hospitali, nyumba za ibada, sehemu za michezo na mapumziko. Mengine ni maeneo ya usalama wa mji kama kituo cha Polisi na Zimamoto, viwanda vidogo vidogo na maeneo ya wazi.

"Katika viwanja hivyo 1,913, shirika limetenga viwanja 1,601 kwa ajili ya kuviuza sawa na asilimia 84 na 313 limevihifadhi sawa na asilimia 16 kwa ajili ya uendelezaji wa baadaye," alisema.



Diwani wa Kata ya Mirerani, mkoani Manyara, Salome Mnyawi (kulia), akimwonesha Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Fakii Lulandala (wa pili kushoto), maeneo yanayoathiriwa na mafuriko kipindi cha mvua, alipotembelea katika kata hiyo, jana. Kushoto ni Diwani wa Kata ya Endiamtu, Lucas Zacharia. **PICHA: GIFT THADEY**

## Wamasai wachangamkia ufugaji kuku, nyuki

**Na Godfrey Mushi,** LONGIDO

JAMII ya wafugaji wa Kimasai wilayani hapa Mkoa wa Arusha imeanza kubadili mfumo wa maisha yao kiuchumi kwa kupunguza ng'ombe, kondoo na mbuzi kwa kuchangamkia ufugaji nyuki na kuku baada ya kubaini inalipa kiuchumi.

Mabadiliko hayo, yamesaidia baadhi yao kuacha kujihusisha na biashara haramu ya ujangili katika hifadhi za wanyamapori na uharibifu wa mazingira kwa kukata miti kwa ajili ya biashara ya kuni na mkaa.

Akizungumzia na Nipashe katika mahojiano maalum jana kuhusiana na mabadiliko hayo, Mkazi wa Kijiji cha Kimokouwa, Losinyati Lendeipa, alisema ufugaji wa nyuki, umewatoa wafugaji hao katika biashara haramu kwa kupata fedha za kutosha kujikimu kimaisha, kusomesha watoto na kuajiri kwa kuzalisha miradi mingine.

'Sisi ni wanufaika wa mradi wa nyuki tuliopata mafunzo kutoka Mradi wa Land For Life, unaotekelezwa na Shirika la WWF (Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira). Tulipata mradi huu kwa ajili ya kunusuru uharibifu wa mazingira kwa kukata miti ovyo, kuchoma mkaa, ujangili na uwindaji haramu wa wanyamapori," alisema Lendeipa na kuongeza kuwa.

"Tumenufaika kwa kupewa hiyo mizinga, na kwa kweli ufugaji huu umetusaidia sana. Tunatarajia kurina asali iliyoko kwenye mizinga wiki hii na tutavuna kiasi cha lita 1,200. Kwa makadirio yetu tutakapoenda kuiuza hiyo asali tunapata Sh. milioni 1.2.

Alisema asali hiyo wataiuza na mazao ya nyuki, mfano masega watatengeneza kupata nta, sabuni dawa za kuchua mwili, kutibu mdomo uliopasuka na mafuta ya kupaka mwilini.

Mkazi wa Kimokuwa, Peipei Laizer (25), alisema ufugaji wa nyuki umewasaidia kujiinua kiuchumi wanawake wa Kimasai.

"Tunaweza kuwasomesha watoto wetu katika shule za mchepuo wa Kingereza na shule za umma na tunaendeleza biashara zetu ndogo ndogo kutokana na fedha tunazopata kupitia ufugaji wa nyuki na kuku.

Biashara nyingine tunazofanya kwa kutumia kipato cha mauzo ya kuku ni kuuza sukari, majani ya chai, mayai na chumvi huku vijijini," alisema Peipei.

Pamoja na mambo mengine, alisema nyuki wanasaidia katika mashamba yao kwa kuchavusha mazao.

Nagelii Losinyati (33), Mkazi wa Kimokuwa, alisema lengo la kuanzisha mradi wa nyuki ni kuwafundisha wenzao namna ufugaji nyuki na kuku, unavyoweza kubadili maisha yao kiuchumi.

Akifafanua zaidi kuhusu mradi huo, Ofisa Mwandamizi wa WWF, Sarah Namelock, alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wengine ili waachane na uharibifu wa mazingira na kujikita katika biashara ya ufugaji nyuki na kuku kwa kuwa ni rafiki wa mazingira.



# Kizungumkuti cha ukame, wakulima kukosa pembejeo

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WAKULIMA wa mazao ya chakula na biashara wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga mkoani hapa, wameiomba Wizara ya Kilimo kurahisisha upatikaji pembejeo za kilimo na kukabiliana na ukame kwa kukosa mvua za kutosha.

Ombi hilo lilitolewa na wakulima wa Kata ya Salawe wakiwa katika maandalizi ya mashamba kufuatia tangazo la Mamlaka ya Hali ya (TMA) kuhusu uchache wa mvua katika kipindi hiki.

Mkulima wa Salawe, Nyoshi Masalu alisema licha ya kuandaa mashamba, hawana mbegu za kutosha kulingana na hali ya hewa, hivyo wanaiomba serikali kuwawezesha kupata mbegu, mbolea na dawa muhimu kwa ajili ya kuua wadudu, magugu na kustawisha mazao.

Alisema amelima ekari 20 na kwa ajili ya kupanda mazao mchanganyiko, lakini kakwama kwa kusubiria mbegu za mahindi, licha ya kujiandikisha kwa Ofisa Kilimo Kata kwa ajili ya kupata pembejeo.

Alidai kila wanapofuatilia, hawapati majibu ya kuridhisha na kuiomba serikali kuingilia kati.

Modesta Kulwa, alisema kwa mujibu wa TMA, kutakuwa na mvua chache, nchini, hivyo wametumia za kwanza kuandaa mashamba ili kupanda mazao yanayostahimili ukame.

Hata hivyo, alisema wamekosa uungwaji mkono kutoka serikalini kwa kukosa mbegu kama ilivyokuwa msimu uliopita.

Alisema serikali inatakiwa kuwatangazia tarehe rasmi ya kupata mbegu ili wafahamu kwani msimu wa kupanda mahindi unajulikana.

Ofisa kilimo wa Kata ya Salawe, Odetha Mushumbusi, alisema dirisha la mbegu za ruzuku zinazotolewa na serikali halijafunguliwa na amekuwa akifuatilia Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo bila kupata majibu.

Mushumbuzi, alidai hadi sasa hajapata jibu lini dirisha hilo litafunguliwa ili wakulima waweze kupata mbegu na kupanda katika mashamba yao kwa wakati.

Alisema, msimu uliopita aliandikisha zaidi ya wakulima 418 waliojitokeza na kupata pembejeo.

Alisema kwa msimu huu idadi hiyo itakuwa imeongezeka kwa sababau bado wakulima wanaendelea kujitokeza na kujiandikisha licha ya baadhi yao kuandaa mashama mapema.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri hiyo, Edward Maduhu, alisema wanasubiri kupewa utaratibu wa kugawa kwa wakulima mbegu za mahindi zinatolewa kwa ruzuku na kuwataka kuendelea kujiandikisha kwenye ofisi za kata.



Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), Mhandisi Yusuph Katopola (kushoto) na Mkurugenzi Mkaazi wa Kampuni ya GOPAInfra ya nchini Ujerumani, Stefan Doerner, wakionesha mkataba wa Sh. bilioni 9 kwa ajili ya mamlaka hiyo kujengewa uwezo wa utendaji kazi na kampuni hiyo, baada ya kutiliana saini, mjini Shinyanga jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Wahudumu afya waonywa kutumia lugha chafu

**Na Ambrose Wantaigwa,** RORYA

MKUU wa Wilaya ya Rorya mkoani Mara, Dk. Khalfan Haule amewaonya watumishi wa afya kuacha matumizi ya lugha chafu kwa wagonjwa.

Dk. Haule alitoa onyo hilo juzi wakati akikabidhi gari lenye thamani ya Sh. milioni 200 lililotolewa na 'Marafiki wa Rorya kutoka Marekani' kwa Hospitali Teule ya Shirati ili kukabiliana na adha ya usafiri kwa watumishi.

Aliwataka watumishi hao kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa viapo vyao, kuepuka kuomba, kupokea rushwa na kutoa lugha zisizostahili kwa wagonjwa.

Kuhusu msaada huo wa gari, mkuu huyo wa wilaya alisema utawawezesha madaktari, wauguzi na wafanyakazi wengine kuongeza kasi ya kuhudumia wagonjwa hasa katika zahanati za vijiji vya pembezoni.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Bwire Chirange, alisema awali baadhi ya madaktari na wahudumu wa afya walilazimika kutumia gharama kubwa kwa usafiri binafsi kufika katika kituo cha kazi na kuchelewesha huduma kwa wagonjwa.

"Tunawashukuru Marafiki wa Rorya kwa msaada huo ambao utawezesha madaktari na watumishi wa hospitali kufika kazini mapema na kutumia muda mchache kuhudumia wagonjwa wetu," alisema Dk. Chirange.

Alisema lengo kuu la utawala wa taasisi hiyo ya afya ni kutoa huduma za kibingwa kwa wananchi wenye kipato cha chini kwa gharama nafuu.

Mwakilishi wa Marafiki wa Rorya kutoka Marekani, Sale Restler, alisema wametoa msaada huo ili kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali kuboresha huduma za afya nchini.

Hospitali hiyo iliyoanzishwa mwaka 1934 na Wamarekani Wamishionari wa Kanisa la Menonaiti (KMT) kwa sasa asa inamilikiwa kwa ubia na Serikali ya Tanzania kuhudumia wakazi wa wilaya zote za Mkoa wa Mara na mikoa jirani.

## Walimu 'stop' kulima mashamba ya shule

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BAADHI ya walimu wa shule za msingi na sekondari wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga, wamepigwa marufuku kulima mazao kwenye mashamba ya shule na kutumika kuzalisha chakula kwa ajili ya chakula cha wanafunzi.

Amri hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro katika Kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya hiyo wakati akijibu hoja zilizoibuliwa na madiwani hao kuhusiana na walimu hao kugeuza mashamba ya shule zao kwa manufaa yao binafsi.

Mtatiro, alisema walimu hawazuiwi kufanya shughuli za kilimo kama sehemu ya kujiongeza kipato na kupata chakula, lakini kutumia mashamba ya shule ni marufuku.

Alisema walimu wanaotaka kulilima mazao, wanapaswa kukodi mashamba kwa wanakijiji na kuyaacha mashamba ya shule kutumika kwa ajili ya kulima chakula cha wanafunzi.

Mtatiro alitaja hatua hiyo itasaidia kuondoa migogoro kwa jamii ambayo ipo tayari kulima mashamba ya shule ili watoto wao wapate chakula shuleni, hususani kwa wazazi wasiokuwa na uwezo wa kuchangia chakula.

Alisema mgogoro wa namna hiyo umewahi kutokea katika Shule ya Manyada, ambako wazazi waligoma kuchagia chakula kutokana na mashamba hayo kulimwa na walimu wakati wao walikuwa tayari kulima ili watoto wao wapate chakula.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ngassa Mboje, alimuagiza mkurugenzi kwa kushirikiana na watendaji wa kata kuandika barua na kuambatanisha waraka wa kuzuia walimu kulima kwenye mashamba ya shule na nakala kusambazwa kwa madiwani na kusambazwa kwa shule zote ili kumaliza tatizo hilo.

Mthibiti Mkuu wa Ubora wa Shule za Halmashauri hiyo, Joyce Andrew, akijibu maswali ya baadhi ya madiwani katika kikao hicho, alisema waraka kama huo walimu walikabidhiwa na nakala kusambazwa kwenye kata zote.

Awali akiibua hoja hiyo, Diwani wa Nyida, Seleman Segeleti, alisema pamoja walimu kuzuiwa kulima kwenye mashamba ya shule hasa yenye rutuba, katika Shule ya Msingi Nduguti ameshaghaa kuona wakilima tena kwa kutumia trekta na kuibua malalamiko kwa wananchi.



# ama

ALHAMISI NOVEMBA 7, 2024

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**USHINDI KWA NGUVU YA TEKNOLOJIA...**
**Vita vya tembo wanaovamia makazi inavyofanikishwa kwa harufu mbaya**



**KAZI YA WATAFITI KIMATAIFA...**
**Mambo 11 yanayoharibu ubongo kufanya kazi, kumbukumbu finyu**

Ukurasa 14

# Uchambuzi wa Samia akiwa Marekani, Tanzania kugeuzwa ngome ya chakula

## •Ataja njia tatu, anauona mwanga; ateta na bosi MCC

**Na Mwandishi Wetu**

MWISHO wa mwezi uliopita, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ametua nchini Marekani kwa ziara inayohusu usalama wa chakula na akakutana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa taasisi ya Millenium Challenge Corporation (MCC), mwanamama mwenzake, Alice Albright.

Ni mazungumzo yaliyojikita kukuza na kuimarisha uhusiano baina ya pande hizo mbili mnamo tarehe 30 mwezi uliopita, Tanzania ni kati ya mataifa wabia wa asasi hiyo yenye makao makuu nchini Marekani.

Nchi zingine za Afrika wabia wa MCC ni kama : Benin, Burkina Faso, Ivory Coast, Ghana, Lesotho, Liberia, Madagascar, Malawi, Mali, Morocco, Msumbiji, Namibia, Niger, Tunisia na Zambia.

Pia, kuna mataifa wadau kama, Ethiopia, Gambia, Kenya, Liberia, Rwanda na Uganda.

Asasi hiyo ina miaka 20 tangu kuanzishwa, mwasisi wake ni Rais George Bush, ikiwa na makao makuu Marekani na majukumu yake ni kukuza uchumi, kufungua milango ya masoko kwa nchi husika na viwango vya maisha ya wakazi wake.

Ubia wa MCC na nchi zinazochaguliwa unajumuisha pale inaporidhishwa na sera husika, pia kasi yake katika ukuaji uchumi kwa mujibu wa taratibu zake, mhitaji huomba mkopo mahsusi pale mradi anaonadi unapopitishwa.

Rais Dk. Samia amekutana na mkuu huyo wa MCC, huku imepita miezi minane tangu Februari mwaka huu, Naibu Mtendaji Mkuu wa asasi hiyo ya MCC, Chidi Blyden, alipokuwa nchini kukagua maendeleo ya miradi wanayosimamia, sambamba na mipango yao na serikali.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Mtendaji Mkuu wa Millenium Challenge Corporation (MCC), Alice Albright, walipokutana Oktoba 30 mwaka huu, huko Des Moines, Iowa nchini Marekani. **PICHA: MTANDAO.**

Muda mfupi kabla ya kuondoka nchini alikokutana na viongozi wa kiserikali akiwamo Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, Blyden akaitaja Tanzania kuwa mbia wao muhimu, akiwa na kauli:

"Tunatarajia juhudi zetu za pamoja kuimarisha utawala bora kwa upana na ulio endelevu katika maendeleo ya kiuchumi."

Ndani ya ziara hiyo nchini, akakagua miradi ya MCC ya mabadiliko, akiwaelimisha vijana kuhamia maisha ya digitali na fursa za kisera nchini, kwenye mabadiliko kisera yaliyoko kitaifa na kimataifa.

**MJADALA WA CHAKULA**

Akiwa nchini Marekani wiki iliyopita, Dk. Samia akashiriki mjadala maalum wa usalama wa chakula, akiwa kati ya wakuu wa nchi wanne wa Kiafrika waliokaribishwa, wenzake wanatoka Sierra Leone, Madagascar na Nigeria, akafafanua azma ya kuifanya taifa lake ngome ya upatikanaji chakula.

Rais Dk. Samia, akaeleza mikakati ya serikali kuibua mabadiliko makubwa ya kilimo, ikilenga Tanzania kujitosheleza na kuwa ngome ya chakula, njia za kupitia anataja malengo matatu ya msingi, nchi imwejiwekea.

Hayo ni kwa mujibu malekezo yanayorejewa, kwa hatua taifa imezichukua katika kikao kinachohusu chakula, kilichofanyika Dakar, Senegal, Januari mwaka jana.

Sura ya kwanza, anaitaja ni kuifanya Tanzania ipate tija katika kilimo, kuanzia wingi wa bidhaa, hadi ubora wake, iwe inafikika na gharama nafuu.

Aidha, lingine linagusa maboresho katika hifadhi ya chakula hicho kikishavunwa shambani kupunguza kinachopotea katika uzalishaji, akiwa na ufafanuzi kwamba kipaumbele ni kuongezea thamani mazao ya kilimo.

Kwa mujibu Rais Dk. Samia, ni hali itakayoisaidia nchi kuhimili upatikanaji mazao ya chakula na manufaa ya kiuchumi kwa wakulima wa Kitanzania.

Mtazamo huo wa kufanya mageuzi wa uzalishaji hadi kuhudumia bidhaa hiyo, ulionekana kuwagusa wadau wa Kimarekani, katika mjadala huo hata kuvuta tabasamu lao.

Dira ya tatu ya Rais Dk. Samia, inagusa ubunifu wa kuwa na ghala la chakula ikiwa na mitazamo mipana kugusa maslahi yanayovuka mipaka, akieleza matarajio kwamba dira tajwa itafikiwa.

"Hatujafikia malengo, lakini ninachokuhakikishia tuko njiani," anasema Dk. Samia, akieleza serikali imebuni Baraza la Ushauri wa Chakula, lililoundwa kwa mujibu wa maelekezo ya kikao cha maendeleo ya uchumi cha wakuu wa nchi, waliokutana na wataalamu, pia asasi binafsi, huko Senegal.

Jukumu kuu la chombo hicho analitaja ni kuhakikisha hatua inapigwa katika kilimo cha chakula nchini. Rais akiwa na ufafanuzi: "Inafanya kazi nzuri katika kuishauri serikali namna ya kutekeleza kuhusu upatikanaji chakula na usalama wake."

Dk. Samia anasema, dhima ya chombo hicho cha ushauri ni kuhakikisha Watanzania wanapata chakula cha kutosha, salama na chenye viini lishe muhimu.

Katika mjadala huo wa wiki iliyopita ambao Dk.Samia alikuwa mgeni mwalikwa, mwaka huu mada yake imegusa "umuhimu wa ushirikiano kati ya sekta za umma na binafsi, pia kuboresha kilimo barani Afrika.'

Tanzania kwa namna yake, ina-

Inaendelea Uk. 13

MAZINGIRA

## USHINDI KWA NGUVU YA TEKNOLOJIA...

# Vita vya tembo wanaovamia makazi inavyofanikishwa kwa harufu mbaya

## •Staili inayotumika kuwekwa mitego mipakani

**Na Ashton Balaigwa, LIWALE**

***Wiki mbili zilizopita, safu hii ilikuwa na ufafanuzi wa namna matukio ya uvamizi wa wanyamapori katika ardhi ya mkoani Ruvuma. Endelea na simulizi hizo mikoa mingine ya Kusini mwa nchi...***

====

NI asimilia 33 ya ardhi Tanzania, inatajwa kutengwa kwa ajili ya kutunza mifumo ya kiikolojia na mazingira, kuhudumia viumbe, wakiwamo wanyamapori, huku huduma mbalimbali za mazingira zikitolewa hifadhini.

Hivi karibuni kumekuwa kukitokea migongano baina ya binadamu na wanyamapori, hata ikaleta athari kwa binadamu, pia wanyama, ikashia migongano kati yao.

Ni hali inayosababisha watu na maisha mengine kuathiriwa, uharibifu unajitokeza kwa wanyamapori wa maeneo jirani na hifadhi, pia shoroba zao.

Pia, kuna athari za moja kwa moja kwa binadamu, ongezeko la uharibifu wa mali na mazao ikisababisha majeraha kwa wanyamapori, huku kukiwapo matukio ya visasi kwenye hifadhi, kati ya binadamu na wanyamapori; inaishia kujengeka dhana potofu.

Serikali sasa imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti Migongano Baina ya Wanyamapori na Binadamu (2020-2024), unaolenga kuboresha maisha ya watu, wanyamapori na haki za jamii kuendelezwa na ustawi wa uhifadhi.

Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, ni miongoni mwa maeneo yenye migongano ya kibinadamu na wanyamapori, sasa serikali inaunda mradi huo.

Ni mpango unaolenga kupunguza migongano ya binadamu na wanyamapori, wadau muhimu wakiboreshewa uwezo wadhibiti na kutatua tatizo hilo.

**DC LIWALE**

Mkuu wa Wilaya ya Liwale mkoani Lindi Goodluck Mlinga, anataja kinachochangia migongano ya binadamu na wanyama, mojawapo ni eneo kubwa limezungukwa na hifadhi, zikiwamo za Nyerere, Selous na hifadhi za vijiji, jumuiya za hifadhi na maeneo ya uvunaji miti ya mbao.

Anasema maboresho ya uhifadhi wanyamapori yameongezeka kwa kasi; katika vijiji 76, kati yake 64 sasa vina changamoto ya uvamizi wa tembo waliko, pia mashamba yao yakaibua migongano ya binadamu na wanyamapori.

"Wilaya yetu ina jumla ya kilomita za mraba 38,000 na eneo kubwa limezungukwa na hifadhi.

"Tuna hekta zaidi ya milioni 2.5 za uvunaji wa miti ya mbao na tunapata faida kubwa kwenye uvunaji," anasema Mlinga.

Anataja migongano ya binadamu na wanyamapori imechangia kuwapo miradi ya serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali, yanayowasaidia kumaliza tatizo hilo, ikiwapo serikali ya Ujerumani kupitia Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ).

Katika ulinzi wake hifadhini, GIZ inawasaidia wakazi kukabili changamoto za tembo mashambani mwao, hali inayosababisha migongano na binadamu.

**MKAKATI WA KIJERUMANI**

Mlinga anataja mkakati wa GIZ kupunguza migongano wameamua kuwasomesha vijana kwenye vyuo vya wanyamapori kutoka vijiji 11, vyenye changamoto kubwa kulinda uhifadhi, vilevile kuwasaidia wananchi kukabiliana na wanyamapori wasifanye uharibifu katika mashamba.

Anasema, mradi wa GIZ uko kutatua changamoto hizo, ikaamua kuja na mbinu nyingine kutoa mizinga ya nyuki kwa vikundi waviweke mashambani, ambako tembo wamekuwa wakiingia, kwani nyuki ni adui mkubwa wa tembo.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alipokabidhi fedha za rambirambi, kwa ndugu ya aliyeuawa na tembo wilayani Liwale, kijiji cha Nammaja wilayani Nachingwea, mnamo Julai 2022.

Mlinga anataja changamoto nyingine inagusa wafugaji wengi kuvamia misitu, akisema serikali tayari inayatatua kwa kuwatengea maeneo; hekta 42,000 za wafugaji.

**MRATIBU MIRADI**

Mratibu wa Mradi wa Utatuzi wa Migongano baina ya Binadamu na Wanyamapori kutoka GIZ wilayani Liwale, Deborah Missana, anasema mradi unatumikia vijiji 11.

Anaviorodhesha kuwa: Turuki, Kitogolo, Mtawatawa, Mtawango, Nahoro, Chimbuko, Nanjegeja, Kimbemba, Naluleo, Ngumbu na Mkutano.

Anasema mradi huo umechagua vijiji hivyo kutokana na changamoto za mgongano kati ya binadamu na wanyamapori, baadhi yao mazao yanaliwa na wanyamapori na wengine wanadhuriwa hasa na Tembo.

Deborah anasema, mafanikio ya mradi huo sasa yapo katika hatua mbalimbali, ikiwamo kuwafundisha wahifadhi kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), jumla ya wahifadhi 15; kati yao wanne walitoka wilaya ya Liwale.

Mratibu huyo wa GIZ, anafafanua kuhusu mafunzo hayo kuwa: "Tunakusudia kutumia teknolojia ya kufukuza tembo wavamizi kwa Ndege Nyuki ndio maana tumewapeleka kwenye mafunzo."

Anaorodhesha mafanikio yanajumuisha kufundisha askari wanyamapori wa vijiji vyote 30 mradi unakopatikana, wakiwamo wasichana 10 na wanaume 20, watakaotoa msaada vijiji humo, pale wanyama waharibifu watakapovamia.

"Pia, tumeweza kutoa mafunzo ya kufundisha Jamii njia ya utatuzi wa Mgongano wa Binadamu na Wanyamapori kwa Lugha ya picha na Michoro ili wenyewe wawe kama wakufunzi kwa wenzao..." anasema mratibu huyo.

Deborah anasema, mafanikio makubwa sasa ni kwa mradi kufanikiwa kufundisha njia mbadala ya utatuzi wa mgongano ya kupika dawa ya harufu ya uzio kufukuza tembo wasiingie shambani.

"Hiii njia ya kupika dawa ya harufu mbaya ya uzio imeonyesha mafanikio kwenye utafiti..." anasimulia na anaongeza:

"Tulianza kufundisha maafisa ugani wa vijiji na baadae kufundisha wana vijiji zaidi ya 1000."

Mratibu huyo anataja mbinu nyingine, wanawafukuza tembo mashambani kwa mizinga ya nyuki, nayo GIZ imeshatoa mizinga 100 Liwale, hali kadhalika wanatarajia kuongeza 200.

"Hiyo Mizinga itawekwa kwenye mashamba yanayovamiwa na tembo. Wote tunajua tembo na nyuki hawapatani, kwahiyo akifika tu kwenye shamba anakutana na hao nyuki na kuondoka eneo hilo mara moja" anasema Mratibu Deborah.



Namna ilivyo udhibiti wa tembo sasa katika makazi ya watu wilayani Liwale.

**UZIO UNAONUKA**

Ofisa Ujirani Mwema kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) Kituo cha Selous Liwale, Aloyce Assenga, anasema teknolojia ya kutengeneza uzio wa harufu mbaya waliofundisha wananchi wa vijiji 11 wilayani Liwale, Lindi umezaa matunda.

Anataja katika Pori la Akiba la Selous, limesaidia kufukuza tembo waharibifu wa mazao mashambani, hata ikapunguza migongano ya binadamu na wanyamapori.

Ofisa huyo anaeleza mbinu hiyo imeanza kupunguza wanyama hao na hasa tembo, wanapoona uzio huo wenye harafu inayowasumbua, hivyo wanaamua kutoingia tena mashambani kufanya uharibifu.

Assenga anafafanua kuwa, ni dawa yenye harufu inayowakera wanyama, iliyotengenezwa kupitia mradi shirika la GIZ, mdau mkubwa wa TAWA na sasa umeonyesha matokeo chanya kwenye vijiji hivyo 11.

"Baada ya kutengeneza harufu mbaya kwenye uzio, tulienda kwa ajili ya kupata mrejesho na kiukweli.

"Jamii imeonyesha waziwazi mapokeo chanya kuwa inasaidia kufukuza wanyama wakali hasa tembo katika mashamba" anasema.

Assenga, ambaye pia ni Ofisa Mhifadhi Wanyama Daraja la Kwanza, anataja ushirikiano baina ya TAWA na mradi wa GIZ, wametoa ufadhili wa mafunzo kwa Askari Wanyamapori wa Vijiji, ili wasaidiane na wale wa TAWA kudhibiti tembo wasiingie mashambani.

Anasema, askari hao wanyamapori vijijini wanapatiwa vifaa zikiwamo mabomu, tochi na pikipiki zinazowasaidia kufika haraka kwenye maeneo yanaripotiwa uvamizi wa wanyama, hata kabla askari TAWA hawajafika.



Mkuu wa Wilaya ya Liwale, Goodluck Mlinga. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**



**WATAALAMU KILIMO**

Ofisa Kilimo anayeshughulikia mradi wa GIZ wilayani Liwale, Anthony Kawishe, anasema kuwepo changamoto ya uvamizi wa tembo mashambani mwa wakulima, wamekuja na mradi wa kukabiliana na migongano hiyo ya binadamu na wanyamapori.

Anaitaja ni kwa shirika la GIZ, inatoa mafunzo kwa maofisa ugani wa vijiji 11 vya mradi wa namna ya kutengeneza harufu mbaya ya uzio; nao wakatoa mafunzo kwa wananchi vjijini mwao.

Baada ya kufunza, kila kijiji kilitengeneza harufu mbaya ya uzio mashambani na kusaidia maeneo mbalimbali, ikiwamo kwa wakulima wa mpunga, hata tembo waliondoka na hawajarudi tena katika mashamba hayo.

Ofisa Ugani wa Kijiji cha Turuki, Kata ya Mihumo, Liwale Mjini, Yunufu Luwongo, anasema mradi wa GIZ umesaidia kuwatengenezea dawa ya harufu mbaya kwenye Uzio inapowekwa mashambani, yakiwa na ufanisi, tembo hawaingii tena.

Anasema kupitia mradi huo, GIZ imeshatoa mafunzo kwa vijana watatu kwenda katika Chuo cha Askari Wanyamapori wa Vijiji, ili awadhibiti wanyama waharibifu na tayari wameshahitimu na kuanza kazi hiyo katika kijiji hicho.

Mkulima wa Kijiji cha Mtawatawa, Nasoro Gochigochi, anaomba utalaam huo wa kutengeneza uzio wa harufu mbaya uenezwe katika vijiji vingine wilayani Liwale, kwani umeonyesha mafanikio makubwa kuwadhibiti tembo wanaofanya uharibifu.

Askari wanyamapori wa vijiji hivyo waliofunzwa, wakiwamo Radhia Abdallah wa kijijini Turuki, anaomba serikali iwapatie vifaa vinavyowasadia kuimarisha ulinzi vijijini, pia pikipiki inayowawahisha katika eneo la tukio, inaporipotiwa uvamizi wa wanyama mashambani.

Radhia anataja tabia ya tembo, kuwa wakali na wao wanapaswa kuwa na vifaa vya kisasa wanapowafukuza, kutoka wanapovamia mashamba ya wakulima na kufanya uharibifu.

Mkurugenzi wa Chama Cha Waandishi wa Habari wa Mazingira (JET), John Chikomo, anasema chombo chao kimetoa mafunzo kwa waandishi wa habari na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini, namna ya kuripoti kwa usahihi Migongano ya Binadamu na Wanyamapori.

Chikomo anasema, mradi huo unapunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori nchini, ikiwagusa walengwa.

Hao ni wakazi wa vijiji vilivyopo Kusini mwa Hifadhi ya Nyerere na Pori la Akiba la Selous katika wilaya za Liwale Mkoani Lindi, Namtumbo na Tunduru mkoani Ruvuma wakilenga kuboresha uwezo wa wadau nchini wanaohusika na kudhibiti.

## UCHAMBUZI WA SAMIA AKIWA MAREKANI, TANZANIA KUGEUZWA NGOME YA CHAKULA

**Inatoka Uk. 11**

tajwa kuwa na faida ya ziada katika ardhi yenye rutuba na wajuzi wa kazi za shamba, wanaotajwa kuwa vivutio kwa wawekezaji wa sekta hiyo.

Pia, Dk. Samia, akawa na fursa ya mjadala wa faragha na maofisa wa serikali, pia taasisi binafsi za Marekani akinadi fursa za kilimo nchini Tanzania, hadi mnyororo mzima wa thamani wa kilimo uliopo nchini.

Rais akawasisitizia haja ya kushirikiana nao, hata Tanzania ichukue nafasi kimataifa kuwa mstari wa mbele katika kukabili njaa na utapiamlo duniani.

**KIKAO CHA DAKAR**

Ni mkutano uliofanyika mwezi Januari mwaka jana, jijini Dakar, Senegal ukiwakusanya wakuu wa nchi mbalimbali kuwataka waandae rasilimali zao na wadau wa maendeleo kuwekeza katika sekta kilimo kuzalisha chakula.

Hiyo inaendana na kuondoa vizingiti vyote katika maendeleo ya kilimo, ikisaidiwa na miradi mipya barani Afrika iongezeke kila mwaka kwa kiwango Dola za Marekani Trilioni moja, ifikapo mwaka 2030.

Hapo inajumuoshja mitazamo inayogusa maboresho ya miundombinu, mifumo ya hali ya hewa, ikiwamo mitaji binfasi inayowaunga mkono kuongeza thamani ya chakula n ahata kuongeza kapu la chakula.

Tafsiri pana inayojengwa hapo ni kuanzia wawekezaji wanaotimiza makubaliano yao na serikali, wakizama katika mfumo wa ubia wa kuzalisha chakula, wakishirikiana na wakuu wa kibenki na wizara zenye dhamana za kilimo, wadau binafsi na taasisi za kifedha.

AFYA

## KAZI YA WATAFITI KIMATAIFA...

# Mambo 11 yanayoharibu ubongo kufanya kazi, kumbukumbu finyu

Na Mwandishi Wetu

SHULE ya Kitabibu ya Harvard, ambayo ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Havard, wakishirikiana na Taasisi ya Kitaifa ya Marekani ya Magonjwa ya Mifumo ya Mishipa, pia Shinikizo zimetafiti na kuja na majibu yafuatayo.

Hapo, imeorodhesha mambo 11 katika ubongo wa binadamu, ambayo yanapopewa nafasi huweza kuleta athari, kama vile hali ya kuwa na usahaulifu.

Mosi, ni kukosa usingizi unaotosha: Kwa mujibu wa Kituo cha Sayansi ya mfumo wa neva (Neurology) cha Marekani, uharibifu mkubwa wa ubongo unasababishwa na kutokuwa na usingizi wa kutosha.

Usingizi wa kutosha kwa watu wazima unamaanisha ni saa saba hadi nane, kati ya saa 24 kwa siku. Wataalamu wanasema kulala mfululizo usiku ni bora zaidi, kwani ubongo unapumzika na kuunda seli mpya wakati wa kulala kwa saa saba na zaidi.

Ili kufanya hivyo, mtu anahitaji wakati anajiandaa kwenda kulala angalau saa moja kabla, asitumie kifaa chochote wakati huo, anasafisha chumba chake na uso usifunikiwe anapolala, kwani kunadhibiti mwenendo wa kutumia hewa ya Oksijeni mwilini.

Pili, kifungua kinywa: Hicho ndicho kinachotoa nishati ya kufanya kazi siku nzima. Kutotumia huko kunapunguza viwango vya sukari kwenye damu, hata kuathiri uwezo wa ubongo.

Tatu, kutokunywa maji ya kutosha: Asimilia 75 ya ubongo ni maji. Hivyo, kuiweka katika hali ya unyevu ni muhimu kwa utendaji wake. Ukosefu wa maji husababisha tishu za ubongo kupungua na seli kupoteza kazi.

Wataalamu wanashauri mtu mzima anapaswa kunywa walau lita mbili za maji kwa siku.

Nne, ni msongo wa mawazo uliozidi: Kuwa na hali hiyo kwa muda mrefu, husababisha seli za ubongo kufa na sehemu ya mbele ya ubongo kusinyaa, ikiathiri kumbukumbu na uwezo wa kufikiria.

Jamii inashauriwa kuepuka majukumu ya ziada kadri inavyowezekana.

Tano, matumizi 'vikokotoo' kupita kiasi: Katika kazi za mahesabu madogo, yanafaa kufanyika bila ya kutumia vikokotoo. Kusoma vitabu na yanayofanana na hayo, kunatajwa kuimarisha ujuzi wa akili ya binadamu.

Tabia hizo zinatajwa kuwa mazoezi ya ubongo, ambayo huweka nguvu zake za kufikiri na kumbukumbu imara kwa muda mrefu.

Kando na hiyo, mtu anaweza kucheza michezo tofauti ya shughuli za ubongo, kama kucheza



Msongo wa mawazo unatajwa kuchangia madhara ya ubongo na kumbukumbu.

ujumbe wa maneno, kulinganisha mafumbo.

Sita, kutumia vipokea sauti kila wakati, pia kusikiliza muziki wa sauti kubwa: Sauti inayoingia masikioni kwa vinavyobanwa kichwani zina madhara.

Pia, kusikiliza kwa sauti kubwa au kwa muda mrefu kwa kelele kubwa, nako kunasababisha atahari.

Mtu uwezo wake wa kusikiliza unapoathrika, unatajwa hakurekebishiki na inakuwa na amdhara hata katika kazi ya ubongo na kumbukumbu.

Kunashauriwa, mtu anaposikiliza nyimbo kwa kutumia vipokea sauti masikioni kwa muda mrefu, asiongeze sauti zaidi ya asilimia 60. Pia, asisikilize mfululizo, ajipe mapumziko walau kwa saa moja.

Saba, kuna mtazamo wa mtu kukaa pekee muda mrefu, hachangamani na wengine: Kuzungumza na watu kunatajwa muhimu kwa afya ya ubongo na kutumia muda mrefu uko pekeee ni mbaya kwa ubongo wako, sawa na kutopata usingizi wa kutosha.

Mjumuiko na marafiki na familia huweka akili safi. Upweke unatajwa kuongeza hatari ya wasiwasi na shida ya akili.

Kuweka ubongo wako kuwa na afya, mtu anatakiwa kujumuika na marafiki wa karibu au wanamilia kila mara, ila wawe wenye mawazo chanya kimaisha.

Nane, kutawaliwa na mawazo hasi: Mtu anapokuwa na tabia ya kuwaza mambo hasi kila wakati, humuwekea mwelekeo wa giza aendako na hata akaangukia hatari kwa afya ya ubongo wake.

Hiyo ni kwa sababu mawazo mabaya, huunda msongo wa mawazo, pia wasiwasi wakati wote, hali inayojilimbikiza ubongo, ambako ndiko kwenye hazina ya kubukumbu.

Mtu anashauriwa kuacha mawazo mabaya anayodumu nayo muda mrefu, kwani inamhatarisha kuwa na tabia aina hiyo. Ikiwa mtu hawezi kubadilika peke yake, anashauriwa kutafuta msaada wa daktari wa akili.

Suala la kuepuka urafiki mbaya unatajwa ni muhimu, hali kadhalika, kuwa karibu au kufuatilia habari mbaya.

Tisa, mtu kuwa na muda mrefu gizani: Utafiti nchini Marekani, umeonyesha kuwa watu wanaotumia muda mrefu gizani au wanatumia muda mrefu katika maeneo yaliyofungwa na hakuna mwanga wa kutosha, pia mzunguko wa hewa, ni mazingira yanawasogeza kwenye shinikizo la ubongo.

Hiyo ni kwa sababu yatokanayo na mwanga wa jua ni muhimu sana kwa ubongo na kufanikisha hilo, mtu anaaswa kupata muda wa kuwapo juani kila siku. Mathalan, nyumbani anaungua milango na madirisha hewa safi na mwanga wa unamfikia.

Kumi, ni kula kula kupita kiasi: Haijalishi aina ya chakula iwe cha afya, au la. Kula kupita kiasi kunaharibu ubongo wa mtu na utafiti unaweka bayana kwamba, ulaji unaopitiliza huziba mishipa ya ubongo na kupunguza mtiririko wa damu.

Hiyo husababisha kupoteza kumbukumbu na kufikiri na shida inafika kwenye akili yake.

Sambamba na hilo, kuna la kula vyakula visivyofaa hasa vya kukaanga, vyenye sukari nyingi zaidi, pia vinywaji baridi, inanagukia hatari kwa ubongo.

Hapo ndiyo inapobeba ujumbe wa umuhimu kuwa na chakula cha wastani na sahihi. Inaelezwa na wataalamu kwamba watu wengi wanadhani kuwa lishe inaishia kuondoa mafuta.

Lakini ukweli unabaki kwamba, asilimia 60 ya ubongo wa binadamu ni mafuta na kila aina ya chakula kinapaswa kuliwa, katika kuujenga, 'kigezo na mashati' vyakula vinapaswa kuliwa kwa kiasi kinachofaa.

Hata hivyo, tahadhari kuu inaangukia hoja kwamba unywaji pombe na uvutaji sigara nao ni hatari kwa afya ya ubongo.

Zinatajwa kuwa na tabia ya kubana mishipa ya fahamu ya ubongo na kuharibu seli na kwa hiyo, eneo la ubongo ambayo ndiyo kumbukumbu inahifadhiwa, haiwezi kukua.

Mwisho, ni kwamba: Watu wanapotumia 'skrini' kwa muda mrefu inatajwa ni kifaa chenye athari kubwa kwa ukubwa na ukuaji wa ubongo.

Pia, utumiaji simu za mkononi kwa Watoto, unatajwa kusababisha uharibifu zaidi kwenye gamba la mbele ya ubongo.

Utafiti unaonyesha kuwa watoto wanaotumia simu zaidi ya saa saba kwa siku wanadhurika. Kwa sababu, kukaa muda mrefu kwenye simu za mkononi kunasababisha shida kama maumivu ya kichwa, kuchanganyikiwa na uvimbe wa ubongo.

Kwa sababu hiyo, 'skrini' wanayotumia watoto inapaswa kuboreshwa. Pia, watu wanashauria wasilale na simu karibu na mwili.

Vilevile, simu inatajwa inafaa kuwekwa kwenye begi badala ya mfukoni. Mtu akiwa anataka kuzungumza kwa muda mrefu, afanyue hivyo kupitia spika, bila kushikilia simu sikioni na kutuma ujumbe wa maandishi, inatajwa ni mbadlka bora kuliko kuzungumza.

• *Kwa mujibu wa BBC*



Chumba anachokaaa binadamu kuwa na mwanga, ni msaada kwa afya ya ubongo wake na kumbukumbu. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



## 'Punguzeni vifo vya wanawake, watoto Singida'

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

WATUMISHI wa afya mkoani Singida wametakiwa kuweka mikakati kwa ajili ya kupunguza vifo vya wajawazito wakati wa kujifungua na watoto.

Rai hiyo ilitolewa jana na Katibu Tawala Wilaya ya Mkalama, Peter Masindi katika kikao cha kujadili vifo vya mama na mtoto mchanga kwa mkoa huo kwa robo ya kwanza Julai 1 hadi Septemba 30 kilichofanyika wilayani hapa.

"Twendeni tufanye kazi kwa bidii ili kuondoa tatizo hili katika mkoa wetu, tutumie vizuri kikao hiki kukabiliana na vifo vya kina mama na watoto wachanga," alisema Masindi.

Aliwakumbusha watumishi hao kuwa na lugha nzuri kwa kina mama wanaofika katika vituo vya afya kupata huduma.

Mratibu wa afya Uzazi na Mtoto wa mkoa huo, Christoweru Barnabas, alisema kupitia kikao hicho watapata ufumbuzi wa namna ya kupunguza vifo hivyo.

Barnabas aliwataka wajawazito mkoani humo kuanza mapema kwenda kliniki ili kuepusha vifo hivyo kwao na watoto wachanga wakati wa kujifungua.

## Katibu mkuu awapongeza wanawake

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum imeupongeza uongozi wa Chama cha Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA) kwa kuelimisha jamii athari za ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake nchini.

Pongezi hizo zilitolewa juzi na Katibu Mkuu wake, Dk. Seif Shekalaghe jijini hapa katika kikao kilichowakutanisha viongozi wa chama hicho na wizara hiyo kujadili ulinzi wa watoto.

Alisema anaupongeza umoja huo kwa jitihada zao kuelimisha jamii kuhusu athari za vitendo vya ukatili wa kijinsia katika jamii.

Shekalaghe, alisema milango ya kushirikiana na WAWATA ipo wazi na wataalam wa wizara yake wapo kurahisisha utekelezaji wa programu za uelimishaji jamii dhidi ya ukatilii wa kijinsia.

Alisema kwa sasa jamii imeelimika kuhusu vitendo hivyo kutokana na watu wengi na wa rika tofauti kuripoti baada ya kutokea katika jamii.

Mwenyekiti wa Chama hicho, Evaline Malisa, akiwasilisha taarifa ya utekekezaji wa miradi kuhusu wanawake na watoto aliiomba wizara hiyo kuwapa idhini kufanya kampeni ya kuelimisha jamii kuhusu athari za ukatili wa kijinsia.

"Kampeni itakayosaidia kuifikia jamii kupitia vyombo vya habari na mikusanyiko ya makundi ya watu ikiwemo ya waumini wa Kanisa Katoliki na maeneo mengine nchini," alisema Evaline.

# Serikali yawaahidi makubwa wachimbaji madini wadogo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeahidi kuendelea kuwatengenezea mazingira mazuri wachimbaji wadogo wa madini nchini ili wawe wachimbaji na wawekezaji wakubwa.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko alitoa kauli hiyo wakati wa uzinduzi wa Jukwaa la Uziduaji Tanzania, lililoshirikisha wadau kutoka ndani na nje ya nchi jijini hapa.

Dk. Biteko, alisema wachimbaji wadogo ni muhimu katika taifa kwa kuwa wana mchango mkubwa kukuza uchumi wa nchi kwa kuchangia pato la taifa.

"Mchango wao unaonekana kwa sasa wanachangia zaidi ya asilimia 40 ya pato la taifa, wanapaswa kuambiwa ukweli ili wazidi kusonga mbele katika uchimbaji wao," alisema na kusisitiza kuwa: "Nchi ni ya kwao, hivyo wanapaswa kunufaika na rasilimali zao."

Biteko, alikwenda mbali zaidi kwa kusema HakiRasilimali wanapaswa kuwaona wachimbaji hao ni watu wa muhimu na kuwasifia kwa mazuri wanayofanya kwenye Sekta ya Madini.

"Jukwaa hili mnapaswa kuwatia moyo na sio kuja na mabaya yao ambayo yanawakatisha tamaa wachimbaji wadogo," alisema.

Aliwataka washirik kutoa maoni kwa uwazi kuhusu matumizi ya nishati safi ili kulisaidia taifa kufikia malengo endelevu waliojiwekea kwa mwaka 2030.

Biteko, alisema wanapojadili ajenda husuani ya matumizi ya nishati hiyo watoe maoni yao kuendana na uhalisia wa Afrika na si kulinganisha na mabara mengine duniani.

"Tunapokutana katika majukwaa kama haya tujadili ambacho kitaleta matokeo chanya kwa taifa, nawasihi mjadili mambo ya msingi yatakayojenga sekta ya uziduaji," alisema Biteko.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dk.David Mathayo, aliiomba serikali kubuni njia mbadala ya kuchimba madini badala ya Zebaki kwa kuwa inaleta changamoto kwa wachimbaji wadogo nchini.

Alisema serikali inapaswa kuongeza teknolojia nzuri na salama zaidi kupata madini badala ya Zebaki.

Mathayo, alisema kwa kusaidia hilo, iwape wachimbaji hao mitaji ambayo itawasaidia kwenye uchimbaji wa madini.

"Naipongeza HakiRasilimali kwa kuandaa majukwaa kama haya kwa sababu yanasaidia kuibua changamoto zilizopo kwenye sekta ya uziduaji," alisema.

Mkurugenzi wa HakiRasilimali, Adam Antony, alisema serikali inapaswa kubuni njia mbadala ya uchimbaji wa madini kwa wachimbaji wadogo ili kuongeza idadi yao.

Antony, alisema matumizi ya Zebaki kwenye uchimbaji madini imekuwa changamoto kwa kundi hilo, hivyo serikali inapaswa kuangalia namna ya kubuni teknolojia zaidi kuwanasua.

Waziri wa Madini, Antony Mavunde, alisema wachimbaji hao wanaendelea kupiga hatua kila iitwapo leo, hivyo serikali itaendelea kushirikiana nao kuhakikisha wanasonga mbele.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego (katikati), akikata utepe kuzindua magari matano yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 795, yaliyotolewa na Serikali kupitia Wizara ya Maji kwa ajili ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Singida jana, yatakayotumika kusimamia shughuli za sekta ya maji mkoani humo. Kushoto ni Meneja RUWASA wa Mkoa huo, Lucas Said. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Kamati yatakiwa kuwawezesha mabinti

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KAMATI ya Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), imetakiwa kuwawezesha kiuchumi mabinti na kuwanusuru dhidi ya ukatili wanaofanyiwa wakati wa kutafuta kazi nje ya Mkoa wa Singida.

Wito huo ulitolewa jana na Katibu Tawala Mkoa huo, Dk. Fatuma Mganga wakati akizungumza na wajumbe wa kamati hiyo kwenye kikao cha kutambulisha mradi unaotekelezwa na Shirika la ESTL kwa ufadhili wa Ubalozi wa Ireland nchini.

Dk. Mganga, alisema umaskini ni sababu kubwa ya ukatili katika familia mbalimbali nchini hususani kwa wanawake.

Ofisa Maendeleo Mwandamizi wa Mkoa huo, Patrick Kasango, alisema mpango wa pili wa MTAKUWWA kitaifa ulizinduliwa Mei, mwaka huu mkoani Dodoma.

Kasongo, alisema mpango huo umezinduliwa kuzuia ukatili, ikiwa ni ajenda ya kimataifa kwa lengo la kufikia usawa wa kijinsia.

Mkurugenzi wa ESTL, Joshua Ntandu, alisema mradi huo unalenga kuziimarisha kamati za kutokomeza ukatili kwenye ngazi zote, kutekeleza majukumu na kutokomeza ukatili mkoani Singida.



# Kipigo cha mume chaua mke

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya, linamshikilia Mkazi wa Maghorofani jijini hapa kwa tuhuma za kumuua mkewe, Emmy Mwasile (35) kwa kipigo kutokana na wivu wa mapenzi.

Akizungumza na wandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Benjamin Kuzaga, alisema mtuhumiwa anadaiwa kumuua mkewe huyo Oktoba 20, mwaka huu kwa kumpiga na kitu kizito mwilini.

Kuzaga, alisema mtuhumiwa huyo inadaiwa kuwa alikuwa anamtuhumu mkewe kuwa na uhusiano wa mapenzi na mwanamume mwingine.

Alisema mtuhumiwa huyo akiwa na mkewe nyumbani kwao, uliibuka mzozo wakati akimhoji kuhusu kuwa na uhusiano na mwanamume huyo.

Alisema wakati wa mzozo, mwanamume huyo alianza kumshambulia kwa kutumia kitu hicho kizito mwilini hadi kufa na kutokomea kusikojulikana kukwepa mkono wa sheria.

Kuzaga, alisema makachero wa jeshi hilo kwa kushirikiana na wa wenzao wa mikoa jirani waliweka vizuizi maeneo mbalimbali yakiwemo ya mipakani na kumnasa mtuhumiwa huyo akijiandaa kutorokea nchi jirani ya Zambia.

"Mtuhumiwa alinaswa na makachero wetu katika mji mdogo wa Tunduma mkoani Songwe akijiandaa kuvuka mpaka kuelekea nchi jirani ya Zambia, baada ya kumkamata alirudishwa hapa (Mbeya) na kuwekwa sero akisubiri hatua za kisheria," alisema.

Wakati huo huo; jeshi hilo linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za kumuua mfanyabiashara wa madini ya dhahabu, Peter Mteta (59), Mkazi wa Matundasi Wilaya ya Chunya kwa kumpiga risasi.

Kuzaga, aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Kenedy Richard maarufu kwa jina la 'Majiulaya' (26), Mkazi wa Kijiji cha Galula Wilaya ya Songwe, Msafiri Mwahonje maarufu Wakwetu (48), wa Matundasi na Uhuru Sukwa Wilaya ya Chunya (63), wa Kijiji cha Magamba Wilaya ya Mbozi.

Alisema watuhumiwa wanadaiwa kumuua mfanyabiashara huyo Oktoba 12, mwaka huu usiku kwa kumvizia akiwa nyumbani kwake na kumpiga risasi nyumbani kwake kisha kutokomea kusikojulikana.

Alisema baada ya tukio hilo kuripotiwa, jeshi hilo lilianza upelelezi na kufanikiwa kuwatia mbaroni watuhumiwa hao Novemba 1, mwaka huu katika Kitongoji cha Ubaruku wilayani Mbarali wakiwa na bunduki iliyotumika kwenye mauaji hayo ikiwa na risasi tano.

Kuzaga, aliwataka wanakazi mkoani Mbeya kufanya kazi halali za kujiingizia kipato na kuacha tabia za kujichukulia sheria mkononi kwa kuwaua watu wasiokuwa na hatia kwa lengo la kujipatia mali.



Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (wa tatu kushoto), akishuhudia shughuli za uchenjuaji madini ya dhahabu kwa wachimbaji wadogo alipofanya ziara katika Mkoa wa Kimadini wa Chunya, mkoani Mbeya hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wanufaika wa TASAF wapewa somo

**Na Mwandishi Wetu,** ILEJE

MKUU wa Wilaya ya Ileje, Farida Mgomi amewataka wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Kata ya Sange kutumia fedha wanazopata kubadili hali ya maisha yao na kujiletea maendeleo.

Mgomi alitoa rai hiyo juzi katika Kata hiyo wakati akizungumza na wanufaika wa mpango huo.

Aliwahimiza wanufaika hao kuwekeza fedha hizo kwa kuanzisha miradi ya ujasiriamali na kujinasua katika lindi ya umasikini ambalo linakwamisha maendeleo.

Mgomi aliwataka wanufaika hao kuonesha kwa vitendo maendeleo waliyofikia badala ya kubaki kama walivyokuwa.

"Hakikisheni mnapiga hatua ya maendeleo ili kuonesha mabadiliko ya fedha mnazopokea kama vile ufugaji wa kuku na wanyama wengine, pia kilimo na biashara ndogondogo," alisema.

Aliwasihi wanufaika hao kutumia njia za mtandao kupokea fedha za mradi huo kwa sababu ni salama na ya uhakika.

Mgomi alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuziinua baadhi ya kaya masikini nchini kupitia TASAF.

**Hakikisheni mnapiga hatua ya maendeleo ili kuonesha mabadiliko ya fedha mnazopokea kama vile ufugaji wa kuku na wanyama wengine, pia kilimo na biashara ndogondogo.**

# Wahamasishwa kupima afya ya udongo bure

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKULIMA wa Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani hapa wametakiwa kupima afya ya udongo wa mashamba yao ili kuongeza uzalishaji wa mazao na kipato.

Wito huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Halmashauri hiyo, Beatrice Tarimo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Beatrice, alisema kutokana na umuhimu wa kupima afya ya udongo, halmashauri hiyo inaendesha zoezi hilo bure.

Alifafanua kuwa kupima afya ya udongo kunasaidia mkulima kujua kiasi cha mbolea anayotakiwa kuitumia kabla ya kulima shamba na kupanda mbegu.

Beatrice, alisema kutokana na udongo wa Njombe kuwa na tindikali kwa kiasi kikubwa, ni muhimu kwa wakulima kupima afya yake ili wazalishe mazao kwa tija na kwa gharama ndogo kutokana na kujua kiasi cha mbolea anachotakiwa kukitumia.

"Mkulima anapopima afya ya udongo maana yake anafanya maamuzi sahihi ni mbolea kiasi gani inahitajika shambani kwa sababu anaweza kupeleka mifuko 10 kumbe shamba linahitaji mifuko mitatu," alisema.

Alitoa rai kwa wakulima wa halmashauri hiyo kuzingatia utabiri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA) kwa kutumia mvua za mwazoni kulima na kupandia, licha ya kuwa za wastani hadi juu ya wastani.

Alisema kuwa kuanzia mwezi huu hadi Januari mwakani kutakuwa na mvua chache.

Baadhi ya wakulima, akiwemo Faraja Luvanda, alisema zoezi la kupima afya ya udongo linatija kubwa kwao kwa kusaidia kuzalisha mazao kwa kwa tija.

Hata hivyo, aliitaka Serikali kuwahisha pembejeo na mbegu katika msimu huu ili wakulima wanufaike.

Halmashauri hiyo imesajIli zaidi ya wakulima 22, 000 kwa ajili ya kunufaika na mbolea ya ruzuku kwa msimu huu wa kilimo wa 2024/25.



# Watalii 800,000 kumiminika Z'bar

**Na Rahma Suleiman, Zanzibar**

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudik Ramadhan Soraga amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) inaendelea kuimarisha ujenzi wa miundombinu ya hoteli ili kukabiliana na kasi ya ongezeko la watalii visiwani hapa kila mwaka.

Soraga, alisema lengo ya serikali hiyo ni kupokea watalii 800,000 kwa mwaka na kwamba linakaribia kufikiwa baada ya Agosti mwaka huu kuvunja rekodi kwa kufikia 72,296 ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka jana walikuwa 53,839.

Waziri huyo aliyasema hayo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume visiwani hapa wakati wa hafla ya mapokezi ya ndege kutoka nchini Uholanzi aina ya Boeing 717-8 Dream Liner iliyotua ikiwa a wageni 305 chini ya Kampuni ya TUI.

Soraga, alisema changamoto hiyo ni fursa ya kuvutia wawekezaji hasa kwenye miundombinu ya malazi kwa kuongeza kasi ya ujenzi wa hoteli za kisasa na kuboresha miundombinu ya zilizopo

Alisema kwa sasa uwekezaji mkubwa wa ujenzi wa hoteli unafanyika katika visiwa vidogo vilivyopo Zanzibar.

Waziri huyo, alisema Zanzibar ni sehemu sahihi na salama kufanya uwekezaji ikiwemo kwenye sekta ya utalii.

Alisema ujio wa ndege hiyo ni ishara nzuri kufikia lengo hilo la kupokea watalii hao 800,000.

Akizungumzia kuhusu changamoto ya malalamiko kuhusu bima ya afya ya wasafiri, alisema huenda imesababishwa na kasi ya uingiaji watalii kuongezeka.

Alisema ndege hiyo kwa muda wa miaka mitano iliyopita ilisita kuleta watalii kutokana na janga la Uviko-19, hivyo kurejea kunaashiria kuthamini juhudi zinazochukuliwa na serikali na kujenga imani kuwa mikakati iliyopo inatengeneza mazingira mazuri kwa wao.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Nadir Abdullatif Yussuf, alisema SMZ itaendelea kuimarisha miundombinu ya usafirishaji ili wageni nchini wapate huduma bora na kuvutia uwekezaji.

Yussuf, alisema mazingira mazuri ni fursa ya kuimarisha uwekezaji na kwamba serikali jukumu lake kubwa ni kuhakikisha ndege nchini zinatua salama na kuhudumiwa vizuri na wageni.

Alisema wanaendelea kujenga jengo la pili abiria katika uwanja huo ili kuhakikisha wageni wanakuwa salama na kuwapatia huduma ya kimataifa.

Naibu Balozi wa Uholanzi nchini, Marrielle van der Linder, alisema ujio wa ndege hiyo ni kufungua fursa za utalii na uchumu visiwani hapa.

Meneja Mkuu wa TUI, Arif Mazrui, alisema ujio wa wageni visiwani hapa unamaanisha kuwa ni kituo bora cha utalii na kuna fursa nyingi.

## Leseni za biashara kutolewa kidijitali

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban amesema upo mkakati wa serikali kuanzisha mfumo wa utoaji wa leseni za biashara kidijitali ili kuondosha urasimu.

Alisema hayo wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuelezea mafanikio ya miaka minne ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi tangu aingie madarakani.

Alisema mfumo huo utarahisisha upatikanaji wa leseni pamoja na kuondosha msongamano kwa wafanyabiashara.

Alisema kwa njia hiyo itaondoa ubabaishaji kwa wafanyabiashara kupata leseni kinyume na sheria baada ya kuingizwa kwenye mfumo.

Akizungumzia mafanikio ya pato litokanalo na uanzishwaji wa viwanda nchini, alisema umefikia asilimia 20 kutoka asilimia 19.6 kabla ya Dk. Mwinyi kuingia madarakani.

Alisema kuwepo kwa eneo maalum la viwanda kutawarahisishia wafanyabiashara wa Zanzibar kuuza bidhaa wanazozalisha na kuunganishwa moja kwa moja na masoko ya kimataifa.

Waziri Shaaban, alisema malengo ya serikali ya kuanzisha viwanda ni kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi, kuongeza usafirishaji wa bidhaa, kutumia malighafi ya ndani, ajira na mapato ya serikali.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, imeendelea kuchukua juhudi kuhakikisha sekta ya viwanda inaimarika kwa uzalishaji wa viwandani kuongezeka.

"Wizara imeanzisha maeneo maalum ya viwanda Dunga kwa Unguja na Chamanangwe kwa Pemba kuandaa mpango wa matumizi kwa maeneo hayo", alisema.




Naibu Waziri wa Afya Zanzibar, Hassan Khamis Hafidh (wa tatu kushoto), akizungumza wakati akifungua mafunzo kwa madaktari yaliyoandaliwa na wizara hiyo kwa kushirikiana na Hospitali ya Watoto ya Hunan ya nchini China, katika Hospitali ya Lumumba, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wizara, washirika kuboresha afya za wananchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema itaendelea kushirikiana na washirika wakiwemo wa nchini China kuboresha afya za wananchi visiwani hapa kwa kupata matibabu sahihi.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Hassan Khamis Hafidh alisema kwa kushirikiana na Serikali ya China wataendelea kuwapatia mafunzo wataalamu wa afya hasa wa watoto kwa lengo kuongeza ujuzi na kupunguza vifo vya rika hilo nchini.

Akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo madaktari na wauguzi wanaotoa huduma za watoto yaliyoandaliwa na Serikali ya China kwa kushirikiana na wizara hiyo katika Hospitali ya Mkoa Lumumba, alisema lengo ni kuhakikisha wanapata ujuzi wa kisasa na mbinu bora za usimamizi wa huduma kwa watoto.

Alisema kupitia elimu hiyo wataimarisha huduma kwa watoto wanaopata matatizo ya kiafya na washirika hao wa maendeleo wakiwemo Hunan Children Hospital ya China kuanzia ngazi ya vituo vya afya hadi hospitali za wilaya na mkoa.

Naibu Waziri huyo, aliwataka madaktari na wauguzi wanaopatiwa mafunzo hayo kuchangamkia fursa hiyo ili kuleta mabadiliko katika utoaji wa huduma.

Kaimu Balozi mdogo wa nchi hiyo Zanzibar, Zhang Min, alisema wamejipanga kuchukua hatua za ziada kusaidia Zanzibar tatizo la vifo vya watoto kwa kuendelea kutoa mafunzo kwa watendaji wa sekta ya afya.

Min alisema China imetoa nafasi 200 kwa madaktari na watendaji wa afya kwenda kujifunza nchini humo ili wananchi wa Zanzibar wapate matibabu sahihi na kuimarika huduma za afya kulingana na miundombinu inayoendelea kujengwa na serikali.

Mkurugenzi Kinga na Elimu ya Afya Zanzibar, Dk Salim Slim, alisema ushirikiano baina ya nchi hizo kwenye sekta ya afya unaendelea kutoa matokeo mazuri kwa pande zote.

Makamu wa Rais wa Hospitali ya Watoto ya Hunan nchini China, Dk Shuang Quan, alisema wataendelea kukuza ushirikiano huo kwa kuimarisha huduma za afya hasa watoto.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**LISA ELIMO MBOWE,** Anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye Index namba **S0248/0656/2019** kilichotolewa na baraza la Mtihani la Taifa kupitia shule ya **MARIAN GIRLS HIGH SCHOOL** mwaka 2019 Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi **PHQ/DAR/ILA/238281/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DIANA EMANUEL SHIJA** Anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index namba **S1235-0017** kilichotolewa na baraza la Mtihani la Taifa kupitia shule ya **MPERA SEKONDARY SCHOOL** mwaka 2018 Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi **PHQ/SHI/KAH/10356/2024**

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**CHRISTINA REGINALD TEMU**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC 784 DGH** Chasses Namba **MD6M14PA1M4N03533,** Engine Namba **AK4NM4003294** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Polisi Taarifa :

**PHQ/ KIL/MOS/25384/2024**

## NAMTAFUTA BI. ELIZABETH GONDWE

**MIMI, FADHILI EDWARD KILEWO** WA S.L.P 9600 DAR ES SALAAM MWENYE SIMU **NA. 0767819988** NAMTAFUTA **BI. ELIZABETH GONDWE ALIYENIUZIA KIWANJA NA. 52 KITALU 'C'** KILICHOPO **BOKO** ILI AWEZE KUNISAIDIA KUKAMILISHA TARATIBU ZA KUHAMISHA MILKI HUSIKA MBELE YA MSAJILI WA HATI MKOA WA DAR ES SALAAM.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JOYCE AMONI**, Anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya boxer yenye namba za usajili **MC441CLL,** Chassis namba **MD2A21BYXKWH97264,** Engine namba **PFZWKH53468,** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

TAARIFA YA POLISI:

**PHQ/DOD/DOD/50090/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**STEVEN JOSEPH MSHOMI**

Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki (FEKON) yenye namba za usajili **T546 BTA,** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nayeye.

**PHQ/MOR/KIL/37690/2024**

## TANGAZO LA KAZI/UALIMU

Tunatangaza nafasi za kazi ya ualimu mchepuo wa kingereza kwa masomo yote na madarasa yote kuanzia chekechea Hadi darasa la saba, sifa za chekechea ni certicate au diploma na kwa darasa la kwanza Hadi la saba ni diploma au shahada ya kwanza ya elimu.

**Mawasiliano 0783298900**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ADAM CAESAR POPPE**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA PRADO** yenye namba ya usajili **T256DFZ.** Yeyote atakae iona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi

TAARIFA YA POLISI

**PHQ/DAR/KIN/242185/2024**

---

**FOMU MADAI 1-3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**

**Kituo cha KATORO Mkoa wa GEITA**

**Shauri la Madai/Ndoa Na 155/2024**

**Jina la Mdai KAPAYA DOTTO**

**Jina la Mdaiwa HELENI RICHARD**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**( Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa HELENI RICHARD Simu……………**

**Kijiji/Kitongoji/Mtaa BULENGAHASI**
**Kata KATORO Wilaya GEITA**

**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai) Madai ya fedha Tsh. 4,800,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 12 Mwezi 11 Mwaka 2024 Saa 2:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA BOMA MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na…40/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: SELEMANI SALEHE wa MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA FIKIRI SELEMANI SALEHE**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 26 Mwezi 11 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 6 mwezi 11 mwaka 2024

HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**

**Kituo cha HANETI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na 03/ 2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU DEO G. CHIDOGO WA ITISO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA GABRIEL MSTAMBI**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 22 Mwezi 11 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

**Zingatia:**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

*Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.

* Marehemu hakuacha wosia

* Futa isiyohusika

Imetolewa leo Tarehe 1 Mwezi 11 Mwaka 2024

………………………………………

**HAKIMU**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE & ADMINISTRATION CAUSE No. 27273 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late BARNABAS ANDREA NHONYA**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**ANDREW KITENDYA NHONYA**

**GENERAL CITATION**
**( Made under Rule 75 Probate Rules, Cap. 352 R.E 2002)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 25 Day of 11, 2024

Dated at Dodoma this 5 Day of 11, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**


**website: www.ippmedia.com**

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Marais duniani walivyopokea ushindi wa Trump Marekani



Rais mteule wa Marekani, Donald Trump akiwa na Mkewe Melania Trump (kushoto) na mwanaye Barron Trump (kulia) alipotangaza ushindi kwa wafuasi wake jana. **PICHA:MTANDAO**

**Na Waandishi Wetu**

USHINDI wa kiti cha urais wa Marekani, Donald Trump kutoka Chama cha Republican, umewaibua marais duniani ambao kwa nyakati tofauti wamempongeza wakiwamo marais wa Afrika.

Miongoni mwa marais waliopongeza ushindi huo ni Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, ambaye kupitia ukurasa wake wa X jana alieleza wazi kwamba, ulimwengu unahitaji viongozi zaidi wanaozungumza kwa niaba ya watu.

"Zimbabwe iko tayari kufanya kazi na wewe na watu wa Marekani ili kujenga ulimwengu bora wenye mafanikio na amani zaidi duniani," alisema.

Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, kupitia ukurasa wake wa X aliandika:

"Ninatazamia kuendeleza ushirikiano wa karibu na wenye manufaa kati ya mataifa yetu mawili katika nyanja zote za ushirikiano wetu.

"Katika nyanja ya kimataifa, tunatazamia kwa hamu kushirikiana kwa karibu na Marekani kwenye urais wetu wa G20 mwaka wa 2025, ambapo Marekani itaturithi katika urais wa G20 mwaka wa 2026."

Hadi gazeti linakwenda mtamboni Trump alikuwa na kura 72,005,781 na mpinzani wake, Kamala Harris kutoka Chama cha Democrats, akiwa na kura 66,922,892.

Katika ukurasa wake wa X, Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Somalia, Hassan Sheikh Mohamud, alionesha shauku ya kuendeleza uhusiano baina ya nchi hizo mbili kwa nia ya kukuza amani, usalama na maendeleo.

Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi, alituma salamu zake za pongezi kwa Trump, akisisitiza nia ya DRC kuendelea kushirikiana na kiongozi huyo mpya wa Marekani katika kukuza uhusiano wa nchi hizo.

Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye, alimpongeza Trump, huku akiuita ushindi huo kuwa wa kihistoria, pia akimtakia kheri na fanaka katika uongozi wake.

Naye, Waziri Mkuu wa Uingereza, Keir Starmer, ameelezea ushindi wa Trump kuwa ni wa kihistoria na kusisitiza uhusiano maalumu kati ya nchi zao mbili utaendelea kustawi.

"Ninatarajia kufanya kazi nanyi katika miaka ijayo, kama washirika wa karibu zaidi, tuko bega kwa bega kutetea maadili yetu ya pamoja ya uhuru, demokrasia na biashara.

"Kutoka kwa ukuaji na usalama hadi uvumbuzi na teknolojia, ninajua kuwa uhusiano maalumu wa Uingereza na Marekani utaendelea kufanikiwa pande zote mbili za Atlantiki kwa miaka ijayo," alisema.

Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, alimpongeza Trump na kueleza kuwa wako tayari kufanya kazi pamoja kama walivyofanya kwa miaka minne, kwa amani na ustawi zaidi.

Rais wa Tume ya Muungano wa Ulaya, Ursula von der Leyen, amesisitizia umuhimu wa uhusiano ya Ulaya na Marekani huku Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz, ameeleza haja ya kufanya kazi na Marekani ili kukuza ustawi na uhuru.

Rais wa Uturuki, Recep Erdogan, amemwelezea Trump kama rafiki yake, huku akionesha uhusiano kati ya Uturuki na Marekani utakuwa imara.

Mfalme Abdullah II wa Jordan, amesisitiza umuhimu wa kuimarisha hatua za pamoja za kuhakikisha kuna amani na utulivu wa kikanda na kimataifa, huku Rais wa Misri, Abdel Fattah el-Sisi, ameonesha nia yake ya kufanya kazi pamoja kuleta amani na utulivu katika Mashariki ya Kati.

Emir wa Qatar, Sheikh Tamim bin Hamad Al Thani, naye ameonesha nia yake ya kufanya kazi tena na Trump na kupitia ukurasa wa jukwaa la X amesema:

"Natarajia kuimarisha uhusiano wetu na ushirikiano wa kimkakati na kuimarisha juhudi zetu za pamoja za kukuza usalama na utulivu katika kanda na ulimwengu."

Wachambuzi wa kisiasa kupitia vyombo vya habari kimataifa, kikiwamo Daily Sabah, kinaeleza hasa kuhusu diplomasia na masuala mengine kama uchumi.

Hata hivyo, Trump anakabiliwa na kibarua kikubwa cha suala la mgogoro wa Mashariki ya Kati, hasa huko Ukanda wa Gaza, huku Israel ikiendeleza mashambulizi dhidi ya kundi la Hamas huko Palestina.

Kutotabirika kwake kunaweza kuwa faida - kunawafanya wapinzani wasielewe anachokifikiria.

Ushindi wa Trump unamaanisha uundwaji mpya na mwelekeo wake katika sera ya kigeni hasa barani Afrika, bara linalojikuta katika swali la iwapo itakuwa ni fursa mpya za kiuchumi.

Kunatajwa kuwapo kwa changamoto za kiusalama na ushindani mkubwa wa soko la kimataifa, kati ya Marekani na China, huku Afrika ikiwa katikati.

Kwa viongozi na raia wa Afrika, utawala wa pili wa Trump unaweza kuleta mitazamo tofauti katika uhusiano wa Marekani na Afrika.

Yako maeneo matatu muhimu ambayo utawala mpya wa Marekani unaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa mwelekeo wa Afrika na yanapaswa kuchunguzwa na rais mpya kwanza ni ushirikiano wa kiuchumi; ushirikiano wa usalama na Afrika katika ushindani wa Marekani na China.

**USHIRIKIANO KIUCHUMI**

Utawala wa Trump huenda ukalenga kukuza uwekezaji wa kibiashara wa Marekani barani Afrika kwa kuondoa vizuizi vya udhibiti na kuweka mazingira mazuri zaidi kwa kampuni za Marekani.

Asili ya biashara ya Trump, inapendekeza kwamba anaweza kufuata mikataba ambayo inatanguliza mapato ya mara moja, kama uchimbaji wa rasilimali na miradi ya miundombinu yenye manufaa ya wazi kwa kampuni za Marekani.

Utawala wake unatajwa kuunga mkono uwekezaji zaidi wa sekta ya kibinafsi na programu chache za usaidizi za kiserikali, ikiendana na imani kwamba mtaji binafsi na mikataba ya nchi mbili, itachochea ukuaji haraka.

Hatua hiyo inaweza kunufaisha nchi tajiri kwa rasilimali na zile zilizo na mazingira thabiti ya udhibiti, lakini kuna hatari kama zikiacha uchumi mdogo au zile zisizo na rasilimali kubwa katika hali mbaya.

Trump anaunga mkono Sheria ya Ukuaji na Fursa ya Afrika (AGOA), sera muhimu ambayo imewezesha mauzo ya Afrika katika masoko ya Marekani, kwa miongo miwili na iwapo itaidhinishwa tena mwaka 2025, AGOA inaweza kutoa fursa kwa uchumi wa Afrika, kufikia soko la Marekani.

**USHIRIKIANO KATIKA USALAMA**

Ushirikiano wa kiusalama unasalia kuwa msingi wa uhusiano kati ya Marekani na Afrika, hasa kutokana na vitisho vya kigaidi vinavyoendelea katika maeneo kama vile Sahel, Bonde la Ziwa Chad na Pembe ya Afrika.

Utawala wa Trump huenda ukazidisha shughuli za Marekani za kukabiliana na ugaidi, ukisisitiza ushiriki wa kijeshi kupitia Kamandi ya Umoja wa Mataifa ya Afrika (AFRICOM).

Hata hivyo, mtazamo wa kijeshi unahatarisha kuweka kando sababu kuu za ukosefu wa utulivu, kama vile umaskini, rushwa na ukosefu wa fursa za kiuchumi, hasa ramani ya barabara ya Afrika

**MWELEKEO**

Mwelekeo na mabadiliko katika mienendo ya mamlaka ya kimataifa yanawapa viongozi wa Afrika nafasi ya kuchukua hatamu na kufafanua njia ya bara hilo, kwa uhuru na maono makubwa zaidi.

Kupitia Umoja wa Afrika (AU) na mashirika ya kikanda, mataifa ya Afrika yanaweza kuweka masharti yao wenyewe kwa ushirikiano wa kigeni.

Uchaguzi huo, hauhusu kuchagua upande na zaidi kuhusu kuunda ajenda inayotanguliza mustakabali wa Afrika, mataifa ya kiafrika yanaweza kusisitiza madai yao kwa ushirikiano.

Kwa kuweka vipaumbele vilivyo wazi na kuongoza kwa msimamo mmoja, Afrika inaweza kushirikisha mataifa yenye nguvu duniani sio kama uwanja wa vita, bali kama mshirika anayethaminiwa na mwenye ushawishi.

## Simba Queens yaapa kisasi ikiikabili Yanga

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 4-1 kwenye Uwanja wa Samora, Iringa dhidi ya Ceasiaa Queens, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Yussif Basigi, amesema hawana muda wa kushangilia wala kupoteza badala yake wanajipanga kulipa kisasi wakikutana na Yanga Princess.

Simba Queens itakutana na Yanga Princess katika mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu ya Wanawake itakayochezwa Novemba 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Yanga Princess kwa mara ya kwanza iliifunga Simba Queens katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii iliyochezwa hivi karibuni.

Akizungumza mara baada ya kumalizika kwa mchezo wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Basingi, kocha aliyechukua mikoba ya Juma Mgunda, alisema hata mchezo huo dhidi ya Ceasiaa Queens, walicheza kwa uangalifu ili kutopata majeruhi.

"Tumeshinda mchezo huu kwa mabao mengi pamoja na changamoto ya uwanja kutokuwa mzuri, hatukumiliki mpira vizuri kutokana na uwanja, lakini tulipambana kuhakikisha tunapata ushindi, tungeweza kupata idadi nyingi zaidi kama uwanja ungekuwa mzuri," alisema kocha huyo raia wa Ghana.

Aliongeza wakati anacheza mchezo huo mawazo yake yako katika mchezo unaofuata wa raundi ya nne dhidi ya watani zao, Yanga Princess, na malengo yake ni kupata ushindi tu.

"Ikumbukwe mechi ijayo itakuwa ni dabi ambayo haitakuwa rahisi, tuko tayari kimwili na kiakili, tumejiandaa ili kushinda kwa sababu mashabiki wetu walivunjika moyo siku ile tulipofungwa kwenye Ngao ya Jamii, tunataka kuwafuta machozi," alisema kocha huyo.

Simba Queens ilifungwa kwa penalti 4-3 na Yanga Princess baada ya sare ya bao 1-1 ndani ya dakika 90 za kawaida.

Katika mechi nyingine za Ligi Kuu ya Wanawake nchini, Gets Program ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Bunda Queens, mechi ikichezwa, Kituo cha Ufundi TFF, Kigamboni huku Yanga Princess ikilazimishwa sare ya goli 1-1 dhidi ya Mashujaa FC kwenye Uwanja wa KMC wakati JKT Queens ikiwaadhibu Mlandizi Queens mabao 7-0.

# PAMBA JIJI FC YAZINDUKA, KOCHA WA FOUNTAIN KILIO

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Pamba Jiji ikipata ushindi wake wa kwanza katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, Kocha Mkuu wa Fountain Gate FC, Mohamed Muya, ameomba radhi mashabiki wa timu hiyo kwa kusema ilikuwa ni 'siku mbaya kazini'.

Fountain Gate ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa mkoani, Manyara ilikubali kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Pamba Jiji ya jijini, Mwanza.

Pamba Jiji, imepata ushindi baada ya kucheza michezo 10, ikitoka sare mitano na kupoteza mitano, kabla ya juzi kuweka rekodi hiyo tangu ilipoanza kucheza kwa mara ya kwanza msimu huu.

Klabu hiyo ya Mwanza imerekea katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, ikikaa nje ya ligi hiyo tangu iliposhuka daraja mwaka 2001.

Timu hiyo imeweka pia rekodi ya kushinda kwa mara ya kwanza ikicheza ugenini, huku wenyeji wao Fountain Gate wakipoteza kwa mara ya kwanza kwenye ardhi ya nyumbani.

Muya alisema timu yake haikucheza vyema katika mchezo huo, huku akiomba radhi viongozi na mashabiki wa soka wa Manyara kwa matokeo hayo.

"Yapo matatizo yanayohusiana na sisi, jinsi vijana wangu walivyocheza tumegundua kuna makosa waliyoyafanya, tutakwenda kuyafanyia kazi, lakini ukweli unabaki pale pale tumepoteza mechi kwa mara ya kwanza nyumbani, niwape pole mashabiki na viongozi wa Fountain Gate, imekuwa ni siku mbaya kazini, tunakwenda kujipanga," alisema Muya.

Naye Fred Minziro, Kocha Mkuu wa Pamba Jiji, aliwapongeza vijana wake, akisema wameanza kumwelewa na baada ya muda wataondoka kabisa katika eneo la hatari kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Nawapongeza vijana wangu kwa kufuata maelekezo, kadri siku zinavyozidi kwenda mbele wachezaji wanaimarika, leo (juzi), mmejionea, majukumu niliyowapa wameyafanyia kazi vizuri na unaona tumeshinda, nadhani tumeanza kukaa sawa na mechi zijazo tutafanya vizuri ili tuondoke huku chini tulikokuwa," alisema Minziro.

Licha ya kupanda ushindi, Pamba Jiji haijasogea hata nafasi moja katika msimamo wa ligi, imebakia kwenye nafasi ya 15, ikifikisha pointi nane huku Fountain Gate ikiwa nafasi ya tano kwa kujikusanyia pointi 17, ikicheza mechi 11.

Minziro ametua Pamba Jiji akichukua mikoba iliyoachwa na Mserbia, Goran Copunovic, aliyetimuliwa kutokana na timu kufanya vibaya.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Asha Djafar (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa Ceasiaa Queens, Winifrida Nicholaus, katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Samora mkoani, Iringa juzi. Simba Queens ilishinda mabao 4-1. **PICHA: MTANDAO**

# JKU, Chipukizi kibaruani leo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya JKU SC inatarajia kukutana na Chipukizi FC katika mechi ya raundi ya 10 ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mau B visiwani hapa.

JKU inashuka uwanjani bado ikiwa na hali mbaya huku wapinzani wao, Chipukizi FC nao wamepoteza mechi mbili mfululizo walizocheza Kisiwani Unguja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa JKU, Salum Ali Haji, alisema matarajio ya kila mwalimu ni kuona timu yake inashinda mechi hasa baada ya matokeo mabaya ya michezo iliyopita.

Haji alisema amekiandaa vyema kikosi chake kuhakikisha kinashinda mchezo huo ambao anaaminiutakuwa mgumu ili kuiweka timu katika nafasi nzuri.

Alisema anashuka uwanjani huku akiwaheshimu wapinzani wake kwa sababu ni miongoni mwa timu ambazo zinawachezaji wazuri.

"Huu sio mchezo rahisi, ni mchezo mgumu kila mmoja anapambania kupata alama tatu kulingana na matokeo au mwelekeo wa timu tangu ligi imeanza," Haji alisema.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Mwembe Makumbi FC dhidi ya Junguni United.

## ZISIKUPITE

### SALAH ATAKIWA SAUDIA

KLABU ya Al-Hilal ya Saudi Arabia inataka kumsajili mshambuliaji wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Salah, mwenye umri wa miaka 32, kabla ya Fainali za Kombe la Dunia la Klabu msimu ujao. ***(Mirror)***

### BARCA YAMTAKA SALAH

BARCELONA pia wanataka kumsajili Mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Salah, baada ya mkataba wake wa Liverpool utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. ***(Sport)***

### ROBERTSON KUULA LIVER

LIVERPOOL inapania kufanya mazungumzo ya mkataba mpya na beki wao wa kimataifa wa Scotland, Andy Robertson, mwenye umri wa miaka 30, msimu huu wa joto. ***(Football Insider)***

### CITY MATATANI EPL

KLABU za Ligi Kuu England, zimehifadhi haki ya kutafuta fidia kwa mapato yaliyopotea ikiwa Manchester City watapatikana na hatia ya kukiuka kanuni za fedha za ligi. ***(Times)***

### EDU ALIIKATA ARSENAL

MKURUGENZI wa zamani wa michezo wa Arsenal, Edu alikataa mkataba mpya wa kubakia kwa washikabunduki hao ili kuchukua nafasi ya kule kwa mmiliki wa klabu nyingi wa Nottingham Forest, Evangelos Marinakis. ***(Mail)***

### BRANTHWAITE SOKONI

KLABU ya Manchester United inapanga kumnunua beki wa Everton na Timu ya Taifa ya England, Jarrad Branthwaite, mwenye umri wa miaka 22, msimu huu wa joto. ***(Sportsport)***

### AMORIM KUIBOMOA SPORTING

KOCHA mpya wa Manchester United, Ruben Amorim, anataka kuwasajili wachezaji watatu wa Sporting, beki wa Ureno, Goncalo Inacio mwenye umri miaka 23, mlinzi wa Ivory Coast, Ousmane Diomande (20), na mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres (26), ili kuungana naye Old Trafford. ***(Sacha Tavolieri)***

### MAGUIRE: SIONDOKI UNITED

MLINZI wa Timu ya Taifa ya England, Harry Maguire, mwenye umri wa miaka 31, hana nia ya kuondoka Manchester United ifikapo Januari na anaamini anaweza kupata mkataba mpya ndani ya klabu hiyo. ***(TBR Football)***

### DURAN AKARIBIA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inajiandaa kuwasilisha ombi la kumnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Colombia, Jhon Duran, mwenye umri wa miaka 20, kutoka Aston Villa. ***(Fichajes)***

### CITY KUONGEZA WAWILI

KLABU ya Manchester City inataka kusajili wachezaji wawili wapya katika dirisha dogo la Januari baada ya kuanza msimu huu kwa majeraha. ***(Football Insider)***

### PALMER KUCHUNGUZWA GOTI

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na England, Cole Palmer, atafanyiwa uchunguzi wa goti lake la kushoto wiki hii baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 kuumia katika mechi ya dhidi ya Manchester United ambayo ilichezwa Jumapili iliyopita. ***(Standard)***

## DON SOKA MAGA LAYA



# ANCELOTTI: MADRID INATAKIWA KUJIHOFIA

## ●●●Ni kutokana na kutoonesha kiwango bora katika mechi zake za...

**MADRID, Hispania**

CARLO Ancelotti amesema Real Madrid „inapaswa kuwa na wasiwasi" baada ya kuchapwa mabao 3-1 nyumbani na AC Milan katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ikiwa ni mchezo wao wa kwanza tangu kufungwa magoli 4-0 na Barcelona kwenye El Clasico.

Bao la kichwa la Malick Thiaw liliifanya Milan kuwa mbele kwa 1-0 pale Santiago Bernabeu kabla ya Vinícius Junior kusawazisha kwa penalti, na Alvaro Morata akaifanya Milan kuwa 2-1 kabla ya kwenda mapumziko.

Tijani Reijnders aliongeza bao la tatu kwa Milan kwenye shambulizi la kaunta, na kuifanya Madrid kupoteza mara mbili katika mechi nne za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

„Tunapaswa kuwa na wasiwasi kwa sababu timu haichezi vizuri," alisema Ancelotti akiiambia Movistar.

"Lazima tuwe imara zaidi, tuwe na nguvu zaidi. Tumeruhusu mabao mengi."

Kipigo hicho kinawafanya Madrid kuhangaika katikati mwa ligi katika awamu mpya ya Ligi ya Mabingwa, huku LaLiga wakiwa tayari wako nyuma kwa pointi tisa dhidi ya vinara Barca.

"Sio juu ya kuwa mvumilivu au la, ukweli ni kile unachokiona uwanjani, ambayo ni kwamba tunakosa kitu," aliongeza Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Wasiwasi katika nyakati hizi ni jambo la kawaida. Utakuwa usiku mrefu, lakini hilo ndilo tunalopaswa kufanya, kufikiria kuhusu kuboresha mambo.

"Tumeruhusu mabao tisa katika michezo mitatu na hayo ni mengi sana kwa timu ambayo ilijenga nguvu yake kwenye uimara."

Ancelotti alisema shambulizi la Madrid -- ambalo lilikuwa na Kylian Mbappé na Vinicius Junior kama safu ya pili dhidi ya Milan -- sio suala.

"Tulikuwa na nafasi nyingi," alisema. „Tatizo kwangu sio hilo, labda tulikosa kuwa sawa, lakini shida kuu ambayo tunapaswa kurekebisha ni jinsi wapinzani wetu wanavyotengeneza nafasi kwa urahisi.

"Usipokuwa imara, unapaswa kujipanga zaidi. Huwezi kusema wachezaji wangu ni wavivu, lakini kwa sasa hatuwezi kufanya kazi pamoja kwa ufanisi."

Ancelotti alikanusha kuwa hali katika chumba cha kubadilishia nguo cha Madrid imekuwa mbaya msimu huu, tangu kuwasili kwa nyota Mbappé majira ya joto.

„Hapana, chumba cha kubadilishia nguo ni cha afya," alisema." Kutakuwa na ukosoaji mwingi, kuhusu mtazamo wetu. Wakosoaji wanafikiria nini, lazima tukubali. Hatufanyi vizuri. Tunataka kufanya vizuri zaidi. Kama hivi ni vigumu kufika mwisho wa msimu."

"Kila mwaka, kuna nyakati ngumu ambapo unapaswa kuhangaika, kupigana, kufikiria. Jambo ambalo si la kawaida ni kwamba timu hii ilikuwa na mwendo mzuri, na imeshuka kwa kasi sana.

"Hiyo ni sehemu ya soka. Unapofikiri kila kitu ni sawa wewe kuanguka, lakini jambo zuri kuhusu soka ni kwamba unaweza kuguswa."

Madrid watawakaribisha Osasuna katika LaLiga Jumamosi kabla ya mapumziko ya kimataifa, huku mchezo wao ujao wa Ligi ya Mabingwa watakuwa ugenini dhidi ya Liverpool Novemba 27.

HABARI MICHEZO

# Silva: City imeachwa gizani

**LISBON, Ureno**

KICHAPO cha kushangaza cha Manchester City cha mabao 4-1 wakiwa ugenini dhidi ya Sporting CP kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hapo juzi kimewaacha "mahali penye giza," kwa mujibu wa Bernardo Silva.

Hat-trick ya mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyökeres, iliifanya Sporting kuibuka kidedea na kikosi cha, Pep Guardiola, sasa kimepoteza michezo mitatu mfululizo katika mashindano yote kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2018.

"Mwanzoni mwa kipindi cha pili, tuliwapa nafasi nyingi sana za kuwa pale na kufunga mabao," alisema Silva kiungo wa kimataifa wa Ureno.

"Inasikitisha, kwa sababu tuko mahali penye giza kwa sasa, na kila kitu kinaonekana kinakwenda vibaya hata tunapocheza vizuri.

"Kwa kweli, tunahitaji kuangalia ndani, kuangalia ni nini hatufanyi vizuri na kuanza kuwa bora haraka sana. Vinginevyo itakuwa ngumu sana kwetu."

Ingawa City walio na majeraha hakika hawako katika hali mbaya, mabingwa hao wa England wamepitia wiki ngumu.

Kwanza walitupwa nje ya Kombe la Ligi na Tottenham Hotspur, kisha msururu wao wa kutopoteza mechi 32 katika Ligi Kuu England ukamalizwa na Bournemouth wikendi iliyopita.

Wakati Phil Foden alipowapa uongozi wa mapema huko Lisbon juzi, walionekana wamerudi kwenye gia, lakini wakamaliza vibaya.

Lakini jinsi walivyopoteza udhibiti wa mechi baada ya Gyokeres kusawazisha karibu na kipindi cha mapumziko haikutarajiwa kabisa.

Waliachwa nyuma mara baada ya muda na kisha wakakubali penalti mbili zisizo na maana, zote zikifungwa na Gyokeres.

"Ni mpira wa miguu, na angalia, kama nilivyosema, ni vigumu kupata sababu za kile kinachotokea hivi sasa kwetu," aliongeza Silva.

"Sikumbuki katika misimu saba na nusu timu hii ikipoteza mechi tatu mfululizo, inaonekana kila kitu kinakwenda ndivyo sivyo kwa sasa.

"Ni wazi, tunahitaji kufanya vyema zaidi. Wachezaji wetu waliojeruhiwa wanahitaji kurejea kwa sababu tunawahitaji. Na haitoshi kwa dakika hii."

City, ambao hawakuwa na wachezaji kama Rodri, Jack Grealish, Rúben Dias na John Stones na walianza kwa mara ya kwanza na beki mwenye umri wa miaka 19 Jahmai Simpson-Pusey.

# FIFA yatoa sheria mpya za Klabu Bingwa ya Dunia

**NYON, Uswisi**

TIMU zinazoshiriki Kombe la Klabu Bingwa ya Dunia ya FIFA mwakani lazima ziwasili Marekani siku tatu hadi tano kabla ya mchezo wao wa kwanza, hii ni kwa mijibu wa sheria mpya za mashindano zilizopitishwa juzi.

Hii inawaacha wachezaji wakikabiliwa na kutokuwa na siku za mapumziko kati ya mechi za kimataifa za kufuzu Kombe la Dunia na kuanza kwa mashindano ya Klabu ya Dunia.

FIFA imewasiliana na timu zilizofuzu kwa Kombe la klabu bingwa la Dunia 2025, mashindano ambayo yatashirikisha timu 32 yatakayofanyika kuanzia Juni 15, mwakani, ikiwa na sheria na kanuni zao za mashindano ambayo yatahitimishwa kwa fainali itakayopigwa Julai 13.

Kama sehemu ya sheria mpya zilizosambazwa, klabu pia zimeambiwa lazima ziwe na timu zao zenye nguvu kwenye michezo na kukabiliwa na faini ikiwa watashindwa kufanya hivyo.

Michuano hiyo ambayo ni mradi unaoendeshwa na Rais wa FIFA, Gianni Infantino, imesababisha kuongezeka kwa machafuko ndani ya mchezo huku vyama vya wachezaji na vyama vya ligi vikitishia kuipeleka FIFA mahakamani.

Wachezaji pia wameelezea wasiwasi wao juu ya kiasi cha michezo wanayolazimishwa kucheza na makocha akiwamo, Pep Guardiola, wa Manchester City na Carlo Ancelotti wa Real Madrid wakilalamikia kazi kubwa kwenye vikosi vyao.

Na kukiwa na mapumziko ya kimataifa yaliyopangwa kati ya Juni 6 hadi 10, mwakani kwa michezo ya kufuzu kwa Kombe la Dunia la 2026, msisitizo wa FIFA kwa klabu ni kuwasili Marekani siku tatu hadi tano kabla ya mchezo wao wa kwanza.

Fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya imepangwa kupigwa mjini Munich Mei 31, mwakani, wiki moja kabla ya mapumziko ya kimataifa -- na inaongeza matarajio ya wachezaji kutoka City, Real Madrid na Bayern Munich kutoka fainali ya Ligi ya Mabingwa, kuingia na raundi ya kimataifa ya mechi, na kisha Kombe la Klabu bingwa ya Dunia.

Kanuni za FIFA za Kombe hilo pia zinasema wamiliki hawawezi kuwa na hisa katika klabu zaidi ya moja na timu lazima iwe na kikosi cha wachezaji 26-35, na madirisha maalum ya uhamisho yatafungiliwa kati ya Juni Mosi hadi 10, mwakani.



# DIAZ AMKOSHA SLOT LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

ARNE Slot amesema "nampenda" Luis Díaz kama mashabiki wa Liverpool na Colombia baada ya fowadi huyo kufunga hat trick na kupata ushindi wa mabao 4-0 katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayer Leverkusen iliyochezwa kwenye Uwanja wa Anfield, juzi.

Liverpool wamesonga mbele zaidi kileleni katika jedwali la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kupata ushindi wa nne mfululizo huku Cody Gakpo akifunga bao moja kwa kichwa kwa timu hiyo.

Huku Díaz akipewa nafasi ya kati isiyofahamika na Slot, mchezaji huyo wa kimataifa wa Colombia alifunga mabao matatu ndani ya dakika 29.

Slot alisema anampenda sana Díaz kama mashabiki baada ya kumtazama akifunga hat trick yake.

"Sio tu watu wa Colombia wanampenda 'Lucho,' mashabiki wa Liverpool pia wanampenda," alisema Slot.

"Nilisikia mara nyingi mashabiki wakiimba wimbo wake na kocha anampenda pia."

"Haiwezekani kwa kila mchezaji kucheza kila mchezo. Nina washambuliaji wanne pekee walio na majeraha tuliyonayo na, kwa orodha ya mechi haiwezekani kuwachezesha. Lakini kwangu, 'Lucho' ni mwanzilishi."

Diaz amefunga mabao tisa katika michezo 15 kwenye mashindano yote akiwa na Liverpool msimu huu na kuwa mtu muhimu kwa Slot.

Na alitoa pongezi kwa kocha huyo wa zamani wa Feyenoord kwa kuziba haraka pengo la kocha zamani Jurgen Klopp.

"Mambo yamekwenda vizuri kwa kocha mpya, haikuwa rahisi kwake kuingia na kujaza viatu vya Jurgen Klopp," alisema Diaz.

"Natumani, tutakuwa na kitu cha kuonyesha kwa hilo mwishoni mwa msimu.

"Jambo muhimu zaidi ni pointi tatu katika toleo hili la Ligi ya Mabingwa Ulaya ili tusonga mbele katika mashindano.

"Tuna wachezaji wa hali ya juu uwanjani kote na nilifurahia sana kucheza katika nafasi hiyo leo. Nina furaha kuwa uwanjani.

"Nahitaji kwenda kutafuta mpira huo sasa kwa sababu ninahitaji kuuweka mahali maalum nyumbani."

# KIBU, MSUVA WAREJESHWA STARS KUWAKABILI ETHIOPIA

**Adam Fungamwango na Somoe Ng'itu**

WINGA wa Simba, Kibu Denis na Simon Msuva wa Al Tabala ya Iraq, wamerejeshwa katika kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kwa ajili ya mechi za kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON 2025), dhidi ya Ethiopia na Guinea, imefahamika.

Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Hemed Suleiman 'Morocco' ameita wachezaji 25 kwa ajili ya michezo hiyo miwili huku pia akimrejesha katika kikosi 'mama' beki wa kulia mzoefu nchini, Shomari Kapombe na aliyekuwa kipa chaguo la kwanza, Aishi Manula.

Stars itakutana ugenini dhidi ya Ethiopia Novemba 16, mwaka huu na siku tatu baadaye itakutana na Guinea.

Morocco pia amemwita kwa mara ya kwanza straika wa Mashujaa FC, Ismail Mgunda, ambaye amekuwa na kiwango kizuri katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea hapa nchini.

Nyota wengine walioitwa katika kikosi hicho ni pamoja na Zuberi Foba, Lusajo Mwaikenda, Adolf Mtasingwa, Paschal Msindo, Feisal Salum na Nassor Hamduni kutoka Azam FC, Ibrahim Hamad 'Bacca', Dickson Job, Mudathir Yahaya, na Clement Mzize (Yanga), Metacha Mnata, Habib Khalid (Singida Black Stars) na David Brayson wa JKT Tanzania.

Wachezaji wengine ni Ibrahim Ame (Mashujaa FC), Abdulrazack Hamza (Simba), Novatus Dismas(Goztepe- Uturuki), Abdulkarim Kiswanya (Azam U-20), Cyprian Kachwele (Vancouver Whitecaps- Canada) na nahodha, Mbwana Samatta anayecheza soka la kulipwa katika klabu ya Paok ya Ugiriki.



Mshambuliaji wa Yanga Princess, Arieth Udong (kulia), akijipanga kumtoka beki wa Mashujaa Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzani (TWPL), iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# Singida BS kufanya 'maajabu'

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA Mkuu wa Singida Black Stars, Patrick Aussems, amesema kikosi chake kitafanya 'maajabu' msimu huu kutokana na aina ya wachezaji alionao.

Aussems aliliambia gazeti hili jana anaiona timu yake ikifanya vizuri msimu huu na kutoa ushindani kwa klabu kubwa hapa nchini katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea.

"Nimekuwa hapa Tanzania kwa mika kadhaa, naifahamu Ligi Kuu, najua timu kubwa zilizozeeleka ni Simba, Yanga na Azam lakini naiona timu yangu ikiwa kwenye mwelekeo mzuri, tunaweza tukafanya kitu ambacho wengi hawategemei," alisema Aussems.

Alisema kikosi chake kina wachezaji wenye uwezo mkubwa, wanaojituma na wanauwezo wa kuipa timu hiyo matokeo mazuri katika mechi zao zijazo.

Aliongeza lengo lake ni kuona timu inaendelea kufanya vizuri na kumaliza katika nafasi za juu ili kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa mwakani.

"Hili linawezekana kama tutaendelea kufanya kazi nzuri, wachezaji kujituma na uongozi kufanya kazi yao, hakuna kisichowezekana, naamini tutafanya vizuri," Aussems aliongeza.

Kabla ya mchezo wa jana kati ya Simba na KMC, Singida Black Stars ilikuwa ikishika nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 23 kinindoni baada ya kucheza michezo 10.

## Kaseba 'aipa maua' Kamisheni ya ngumi

**Na Shufaa Lyimo**

MWENYEKITI wa Chama cha Mabondia wa Kulipwa Tanzania (TPBA), Japhet Kaseba, ameitaka Serikali iwaongezee muda wa kufanya kazi Kamati ya Mpito ya Kamisheni ya Ngumi kutokana na kuridhishwa na kazi wanazozifanya.

Kaseba alisema hayo jana, wakati alipokuwa anafanya mazungumzo na gazeti la hili na kuongeza kamati hiyo imetendea haki majukumu waliyopewa.

"Ninaomba Serikali iwaongezee muda kamati ya mpito waliyoiteua baada ya kubaini mapungufu kwa viongozi waliokuwapo sasa hivi, tunafanya kazi kwa kushirikiana bila ya kupata vitisho na kelele tofauti na ilivyokuwa nyuma," alisema Kaseba.

Aliongeza tangu walipoanza kufanya kazi na kamati hiyo, mambo mengi yamebadilika kwa upande wa mabondia ikiwamo kulipwa fedha kabla ya kupanda ulingoni.

"Mabondia watumie vizuri vipaji vyao kwa sababu vinawasaidia kupata ajira na vilevile kuimarisha miili yao, tunaamini kila mmoja atafanya majukumu yake kwa weledi," alisema mwenyekiti huyo.

## Vishale Dar wapania makubwa kimataifa

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Vishale Mkoa wa Dar es Salaam (DADA), kimesema kimejiandaa kufanya vizuri katika mashindano ya Afrika Mashariki (Kenya Open), yatakayofanyika kuanzia keshokutwa hadi Novemba 10, mwaka huu jijini, Nairobi nchini Kenya.

Makamu Mwenyekiti wa (DADA), Kampasi Kibago, alisema walianza mapema maandalizi ya kushiriki mashindano hayo kwa sababu wanataka kupeperusha vyema bendera ya Tanzania.

Kibago alisema mbali na Dar es Salaam, mikoa mingine iliyothibitisha kushiriki mashindano hayo ni Arusha, Dodoma, Uganda na wenyeji Kenya.

"Mchezo huu kwa sasa umeanza kushika kasi tofauti na miaka ya nyuma, watu wameanza kuupenda na kuuelewa. Kwa upande wetu maandalizi yanaendelea vizuri ili kuhakikisha tunakwenda kuiwakilisha vyema nchi yetu, tunakwenda kushindana," alisema Kibago.

Aliongeza mashindano yatashirikisha timu za wanaume na wanawake na lengo lake ni kupata Klabu Bingwa ya Afrika Mashariki.

Michezo
Alhamisi Novemba 7, 2024
Nipashe

Diaz amkosha Slot Liverpool UKURASA 22



# SIMBA SC YAKAA KILELENI LIGI KUU

●●●Ni baada ya jana kupata ushindi mnono dhidi ya KMC, hata hivyo huenda....

**Na Faustine Feliciane**

MABAO ya Awesu Awesu, Jean Charles Ahoua na Edwin Balua dhidi ya KMC jana kwenye ushindi wa mabao 4-0 yaliipandisha Simba kutoka nafasi ya tatu mpaka kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kufikisha pointi 25, pointi moja zaidi ya Yanga ambao leo wana nafasi ya kurejea kileleni kama watapata ushindi dhidi ya Tabora United kwenye mchezo utakaochezwa uwanja wa Azam Complex.

Simba jana walianza mchezo huo kwenye uwanja wa KMC kwa kasi ambapo walikosa mabao dakika ya tatu na ya 17 baada ya Ahoua na Steven Mukwala kushindwa kuzitumia vizuri krosi za beki wa pembeni, Valentin Nouma, hata hivyo walifanikiwa kuibuka na ushindi huo mnono.

Simba walianza kuhesabu mabao yao katika dakika ya 24 kufuatia shambulizi lao lililozaa matunda ambapo Awesu alifunga bao la kwanza kwa shuti la juu akiwa ndani ya boksi baada ya kupokea pasi nzuri ya Mukwala.

Baada ya bao hilo KMC walijaribu kujipanga kulipiza mashambulizi lakini juhudi zao zilikuwa zikizimwa na viungo wa Simba wakiongozwa na Fabrice Ngoma na Fernandez Mavambo.

Zikiwa zimebaki dakika saba kabla ya kwenda mapumziko, Ahoua aliipatia Simba bao la pili kwa mkwaju wa penalti iliyotolewa na mwamuzi Shomari Lawi baada ya Shomari Kapombe kuangushwa kwenye eneo la hatari.

Mabao hayo mawili yalidumu mpaka kipindi cha kwanza kinamalizika.

Kipindi cha pili kilianza kwa kasi ambapo timu zote zilishambuliana huku KMC wakionekana kubadilika kwa kumiliki mpira, hata hivyo ni Simba walioendelea kuzifumania nyavu za wapinzani wao ambapo dakika ya 66, mtokea benchi, Balua aliyeingia dakika ya 60 kuchukua nafasi ya Awesu kuipatia Simba bao la tatu kwa shuti kali akiwa ndani ya boksi baada ya kupokea pasi ya Nouma.

Mbali na Balua, Simba pia iliwaingiza Mzamiru Yassin, Omary Omary na Kibu Denis kuchukua nafasi za Fernandez, Ngoma na Ladack Chasambi mabadiliko yaliyowaongezea nguvu.

Dakika ya 69, makosa ya beki wa KMC, Ismail Gambo yalitumiwa vizuri na Ahoua aliyeipatia Simba bao la nne kwa shuti la chini chini baada ya beki huyo kushindwa kurudisha vizuri mpira wa golikipa wake ambao ulinaswa na mfungaji.

Bao hilo limemfanya Ahoua kufikisha idadi ya mabao matano na ‚assist‘ nne msimu huu akiwa nyuma kwa goli moja dhidi ya kinara wa mabao mpaka sasa, Seleman Mwalimu wa Fountain Gate mwenye mabao sita.




Kiungo wa Simba, Jean Charles Ahoua akishangilia moja ya goli aliloifungia timu hiyo jana kwenye mchezo dhidi ya klabu ya KMC kwenye uwanja wa KMC Mwenge, Dar es Salaam. Simba ilishinda mabao 4-0. **PICHA:BINZUBEIRY**

## Gamondi: Hasira kwa Tabora Utd

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

HAWAPONI, hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Tabora United itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Kauli hiyo inatokana na hasira za kupoteza mechi dhidi ya Azam lakini pia akitaka timu yake ikae kileleni katika msimamo wa ligi hiyo.

Kocha huyo raia wa Argentina, alisema Yanga itacheza mchezo wa kasi na kushambulia muda wote na amewataka wachezaji wake kutumia kila nafasi itakayopatikana ili kupachika mabao yatakayowawezesha kupata ushindi na kuwarudishia furaha mashabiki wao.

“Mechi hii ipo mikononi mwetu, sisi ndiyo tutaamua tucheze vipi, tuwafungue vipi wapinzani wetu, nadhani wao watacheza kwa ajili ya kutuzuia na kuzima mbinu zetu, tunacheza kwa kasi na kutumia nafasi zitakazopatikana ili kuwafungua wapinzani na kuwatoa nyuma ambako watakuwa wamejazana.

Hizi timu kama hujapata bao hawaondoki nyuma, ukitaka ucheze nao vizuri funga kwanza bao, hapo wataanza kutoka na wao kuanza kushambulia, mpira utachezwa vizuri,“ alisema Gamondi.

Kocha huyo aliongeza katika mechi ya leo atawakosa wachezaji wake watatu nyota ambao ni Ibrahim Hamad ‚Bacca‘, Dickson Job na Yao Kouassi kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kadi na majeruhi.

“Tulipoteza mchezo wetu waliopita, lakini huu tutafanya kila tunachoweza ili kurudisha furaha kwa mashabiki wetu, tunataka kushinda ili tuendelee kuongoza ligi wakati tunakwenda katika mapumziko ya Kalenda ya FIFA,“ alisema kocha huyo.

Nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, aliliambia gazeti hili wanarejea katika ligi kwa nguvu baada ya kupoteza mchezo uliopita.

“Tunataka kurejea kwa nguvu, matokeo yaliyopita yamepita, kama wachezaji tupo katika hamasa ya hali ya juu, mashabiki waendelee kutusapoti na hatutawaangusha,“ alisema Mwamnyeto.

Kocha wa makipa wa Tabora United, Khalfan Mbonde, amekiri watakuwa na dakika 90 ngumu dhidi ya Yanga, lakini wamejipanga kisawasawa kukabiliana nao huku Heritier Makambo na Yacouba Songne, wakitarajiwa kuongoza kikosi hicho.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >